



OKTOBA 1, 2010

MNARA WA MLINZI

UNAOTANGAZA UFALME WA YEHOVA

Mambo Saba
Unayohitaji Kujua
Kuhusu **Sala**

KUSUDI LA GAZETI HILI, *Mnara wa Mlinzi*, ni kumheshimu Yehova Mungu, ambaye ndiye Mtawala Mkuu wa ulimwengu. Kama vile minara ya walinzi nyakati za zamani ilivyowasaidia watu kutazama mambo yaliyokuwa yakitendeka mbali, ndivyo gazeti hili linavyotonyesha maana ya matukio ya ulimwengu kupatana na unabii wa Biblia. Linawafariji watu kwa habari njema ya kwamba hivi karibuni Ufalme wa Mungu, ambao ni serikali halisi iliyo mbinguni, utakomesha uovu wote na kuigeuza dunia kuwa paradiso. Linawatia watu moyo wamwamini Yesu Kristo, ambaye alikufa ili tupate uzima wa milele na ambaye sasa anatawala akiwa Mfalme wa Ufalme wa Mungu. Gazeti hili limekuwa likichapishwa na Mashahidi wa Yehova tangu 1879 nalo si la kisiasa. Linashikamana na Biblia ambayo ndiyo msingi wake.

Gazeti hili haliuzwi. Ni sehemu ya kazi ya elimu ya Biblia ulimwenguni pote inayotegemeza kwa michango ya hiari. Isipokuwa iwe imeonyesha vingine, Maandiko yamenukuliwa kutoka katika *Biblia Takatifu—Tafsiri ya Ulimwengu Mpya*.

MAKALA ZA KWANZA

Mambo Saba Unayohitaji Kujua Kuhusu Sala

- | | |
|----------------------------|--|
| 3 SALA Kwa Nini Tusali? | 9 SALA Tusali Wakati Gani na Mahali Gani? |
| 4 SALA Tusali kwa Nani? | |
| 6 SALA Tusali Jinsi Gani? | 10 SALA Je, Inaweza Kutusaidia? |
| 7 SALA Tusali Kuhusu Nini? | 11 SALA Je, Mungu Atasikiliza na Kujibu Sala Zetu? |

SEHEMU ZINAZOCHAPISHWA KWA UKAWAIDA

- 12 Je, Wajua?
- 13 Wasomaji Wetu Wanauliza . . .
- ◀ 14 Igeni Imani Yao
—'Aliendelea Kukua Akiwa na Yehova'
- 23 Mkaribie Mungu
—"Msikiaji wa Sala"
- 24 Wafundishe Watoto Wako
—Ufalme Ambao Utabadili Dunia Nzima

PIA KATIKA TOLEO HILI

- ◀ 19 Jinsi Unavyoweza Kuzuia Hisia Zisizofaa
- 26 Mazungumzo Pamoja na Jirani
—Roho Takatifu Ni Nini?
- 29 Uwezo wa Kusema kwa Lugha
—Je, Unatoka kwa Mungu?



SALA. Kuna mambo machache katika Biblia yanayopendwa na ambayo husababisha udadisi mwingi kama vile sala. Fikiria maswali saba ambayo yanaulizwa kwa ukawaida kuhusu sala, na kisha ujiunge nasi ili kuchunguza majibu yanayopatikana katika Biblia. Makala hizi zimeandaliwa ili kukusaidia uanze kusali au uboreshe sala zako.



1

SALA

Kwa Nini Tusali?

ULIMWENGUNI pote, watu wa kila utamaduni na dini husali. Wanasali wakiwa peke yao au wakiwa kikundi. Wanasali wakiwa katika makanisa, mahekalu, masinagogi, misikiti, au mahali penginepo pa ibada. Wanatumia mika ya kusalilia, rozari, magurudumu ya sala, sanamu, vitabu vya sala, au sala ambazo zimeandikwa katika viba vidogo ambavyo huning'inizwa ukutani.

Sala inawafanya wanadamu wawe tofauti na viumbe vingine vyote duniani. Ni kweli kwamba kwa kadiri fulani tunafanana na wanyama. Kama tu wanyama, tunahitaji chakula, hewa, na maji. Pia tunazaliwa, tunaishi, na kisha tunakufa. (Mhubiri 3:19) Lakini wanadamu pekee ndio wanaosali. Kwa nini?

Labda jibu rahisi ni kwamba tuna uhitaji wa kusali. Kwa ujumla sala huonwa kuwa njia ya wanadamu ya kuwasiliana na ulimwengu wa roho, kuwasiliana na chochote ambacho watu hukiona kuwa kitakatifu na chenye kudumu. Biblia inaonyesha kwamba tuliumbwa tukiwa na tamaa ya mambo hayo. (Mhubiri 3:11) Wakati fulani Yesu Kristo alisema: "Wenye furaha ni wale wanaotambua uhitaji wao wa kiroho."—Mathayo 5:3.

Ni jambo linalopata na akili kwamba 'uhitaji wa kiroho' ndio unaofanya watu wawe na majengo makubwa na vifaa vya ibada vya kale, na kutumia saa nyingi katika sala. Bila shaka, watu fulani hujitegemea au kuwategemea wana-

damu wenzao ili kutosheleza mahitaji yao ya kiroho. Je, huoni kwamba wanadamu hawana uwezo wa kutosheleza uhitaji huo kikamili? Sisi ni dhaifu sana, maisha yetu ni mafupi, na hatuna uwezo wa kujua wakati ujao. Mtu anayeweza kutimiza uhitaji huo, lazima awe mwenye hekima, mwenye nguvu zaidi, na *anayedumu kwa muda mrefu* zaidi kuliko sisi. Ni mahitaji gani hayo ya kiroho ambayo yanatusukuma tusali?

Fikiria hili: Je, umewahi kutamani kupata mwongozo, hekima, au majibu ya maswali yanayoonekana kuwa hayawezi kujibiwa na wanadamu? Je, umewahi kuhisi kwamba unahitaji faraja baada ya kupata msiba mkubwa, au unahitaji kupata mwongozo wa kufanya uamuzi mzito, au kusamehewa baada ya kulemewa na hisia za hatia?

Kulingana na Biblia, hizo zote ni sababu nzuri zinazoweza kumfanya mtu asali. Biblia ndicho kitabu kinachotegemeka zaidi kuhusiana na suala hili, na kina sala za wanaume na wanawake wengi waaminifu. Walisali ili wapate faraja, mwongozo, msamaha, na majibu ya maswali magumu.—Zaburi 23:3; 71:21; Danieli 9:4, 5, 19; Habakuki 1:3.

Hata ingawa sala hizo zilitofautiana, zilikuwa na jambo fulani linalofanana. Wote waliotoa sala walitambua jambo fulani muhimu ambalo lilifanya sala zao zijibiwe, na ambalo linapuuzwa na watu leo. Walijua walipaswa kusali kwa nani.

Tusali kwa Nani?

Je, MUNGU anasikiliza sala zote bila kujali zinaelekezwa kwa nani? Leo, watu wengi wanafikiria hivyo. Wazo hilo linaungwa mkono na watu wanaopendelea kuchanganya ibada na wanaotaka dini zote zikubalike, ijapokuwa kuna tofauti kati ya dini hizo. Hata hivyo, je, inawezekana kwamba wazo hilo si la kweli?

Biblia inafundisha kwamba mara nyingi watu hawaelekezi sala zao kwa Mungu wa kweli. Zamani Biblia ilipokuwa ikiandikwa, lilikuwa jambo la kawaida kwa watu kuelekeza sala zao kwa sanamu za kuchongwa. Hata hivyo, Mungu alionya tena na tena kuhusu zoea hilo. Kwa mfano, andiko la Zaburi 115:4-6 linasema hivi kuhusu sanamu: “Zina masikio, lakini haziwezi kusikia.” Wazo hilo liko wazi. Kwa nini usali kwa mungu ambaye hawezi kukusikia?

Simulizi fulani la Biblia linaeleza zaidi kuhusu jambo hilo. Nabii wa kweli Eliya aliwaambia manabii wa Baali wasali kwa mungu wao, kisha yeye asali kwa Mungu wake. Eliya alisema kwamba Mungu wa kweli angejibu sala lakini yule

wa uwongo hangejibu. Manabii hao wa Baali walikubali kufanya hivyo, nao wakasali kwa bidii kwa muda mrefu, huku wakilia kwa sauti kubwa—lakini hawakufanikiwa! Simulizi hilo linasema: “Hapakuwa na yeyote aliyejibu, wala aliyewasikiliza.” (1 Wafalme 18:29) Lakini ni nini kilichotokea Eliya aliposali?

Baada ya Eliya kusali, Mungu wake alijibu mara moja kwa kutuma moto kutoka mbinguni ili kuteketeza dhabihu ambayo Eliya alitayarisha. Kwa nini sala hiyo ilijibiwa? Kuna jambo moja muhimu katika sala ya Eliya ambayo inapatikana katika 1 Wafalme 18:36, 37. Sala yake ilikuwa fupi sana. Katika Kiebrania cha awali, sala hiyo ina maneno 30 hivi. Hata hivyo, katika maneno hayo machache, Eliya alitumia mara tatu jina la Mungu la kibinafsi, Yehova.

Baali, ambaye jina lake linamaanisha “mmiliki” au “bwana,” alikuwa mungu wa Wakanaani, na kila eneo lilikuwa na sanamu yake ya Baali. Hata hivyo, Yehova ni jina la kipekee, linalomrejelea Mungu mmoja tu katika ulimwengu wote. Mungu huyu aliwaambia watu wake hivi: “Mimi ni Yehova. Hilo ni jina langu; nami sitampa mwingine yeyote utukufu wangu mwenyewe, wala sitazipa sanamu za kuchongwa sifa yangu.”—Isaya 42:8.

Je, sala ya Eliya na zile za manabii wa Baali zilienda kwa yule Mungu wa kweli? Ibada ya Baali iliwashushia watu heshima kwa kuwataka wafanye ukahaba na hata kutoa watu dhabihu. Kinyume cha hilo, ibada ya Yehova iliwakweza watu wake, Israeli, kwa kuwaepusha na matendo hayo mapotovu. Hebu fikiria hili: Ikiwa unamwandikia barua rafiki unayemheshimu sana, je, unaweza kutarajia barua

MNARAWA MLINZI

UNAOTANGAZA UFALME WA YEHOVA

Je, wewe ungependa kupata habari zaidi au kujifunza Biblia nyumbani kwako bila malipo? Tafadhali tuma ombi lako kwa Mashahidi wa Yehova ukitumia anwani ifaayo kati ya anwani zilizo hapa. Orodha kamili ya anwani inaweza kupatikana katika anwani hii ya mtandao www.watchtower.org/address.

America, United States of: 25 Columbia Heights, Brooklyn, NY 11201-2483. **Australia:** PO Box 280, Ingleburn, NSW 1890. **Britain:** The Ridgeway, London NW7 1RN. **Burundi:** BP 2150, Bujumbura. **Congo, Democratic Republic of:** BP 634, Limete, Kinshasa. **Ethiopia:** PO Box 5522, Addis Ababa. **Ghana:** PO Box GP 760, Accra. **Kenya:** PO Box 21290, 00505 Nairobi. **Malawi:** PO Box 30749, Lilongwe 3. **Nigeria:** PMB 1090, Benin City 300001, Edo State. **Rwanda:** BP 529, Kigali. **South Africa:** Private Bag X2067, Krugersdorp, 1740. **Tanzania:** PO Box 7992, Dar es Salaam. **Uganda:** PO Box 4019, Kampala. **Zambia:** PO Box 33459, 10101 Lusaka. **Zimbabwe:** Private Bag WG-5001, Westgate.

The Watchtower (ISSN 0043-1087) is published semi-monthly by Watchtower Bible and Tract Society of New York, Inc.; M. H. Larson, President; G. F. Simonis, Secretary-Treasurer; 25 Columbia Heights, Brooklyn, NY 11201-2483, U.S.A. and in England by Watch Tower Bible and Tract Society of Britain, The Ridgeway, London NW7 1RN (Registered in England as a Charity). Periodicals Postage Paid at Brooklyn, NY, and at additional mailing offices.

© 2010 Watch Tower Bible and Tract Society of Pennsylvania. Haki zote zimehifadhiwa. Printed in Britain.

Semimonthly

SWAHILI



Jambo ambalo Eliya aliwaambia manabii wa Baali wafanye linathibitisha kwamba sala zote hazielekzwi kwa Mungu wa kweli

hiyo ipelekwe kwa mtu mwenye jina tofauti na ambaye ana sifa tofauti na zile za rafiki yako? Bila shaka, hapana!

Ikiwa unasali kwa Yehova, unasali kwa Muumba, ambaye ni Baba ya wanadamu wote.* Nabii Isaya alisali hivi: “Wewe, Ee Yehova, ni Baba yetu.” (Isaya 63:16) Huyu ndiye ambaye Yesu Kristo alimrejelea alipowaambia wafuasi wake: “Mimi ninapanda kwenda kwa Baba yangu na Baba yenu na kwa Mungu wangu na Mungu wenu.” (Yohana 20:17) Yehova ndiye Baba ya Yesu. Huyu ndiye Mungu ambaye Yesu alisali kwake na kuwafundisha wafuasi wake wafanye vivyo hivyo.—Mathayo 6:9.

Je, Biblia inatugiza tusali kwa Yesu, kwa

* Mapokeo fulani ya kidini yanasema kwamba ni kosa kutaja jina la kibinafsi la Mungu, hata katika sala. Hata hivyo, jina hilo linapatikana karibu mara 7,000 katika lugha za awali za Biblia, hasa katika sala na zaburi za watumishi waaminifu wa Yehova.

Maria, kwa watakatifu, au kwa malaika? Hapana—tunapaswa kusali kwa Yehova tu. Acheni tuchunguze sababu mbili za kufanya hivyo. Kwanza, sala ni ibada, na Biblia inasema kwamba ni Yehova pekee anayepaswa kuabudiwa. (Kutoka 20:5) Pili, Biblia inafunua kwamba Yehova pekee ndiye mwenye jina la cheo “msikiaji wa sala.” (Zaburi 65:2) Hata ingawa Yehova amewapa wengine majukumu mengi, hajampa mtu yeyote jukumu la kusikiliza sala. Ameahidi kusikiliza sala zetu yeye mwenyewe.

Hivyo, ikiwa unataka Mungu asikilize sala zako, kumbuka himizo hili linalopatikana katika Maandiko: “Kila mtu anayeliitia jina la Yehova ataokolewa.” (Matendo 2:21) Hata hivyo, je, Yehova anasikiliza sala zote bila masharti yoyote? Au kuna jambo lingine tunalohitaji kujua ikiwa tunataka Yehova asikilize sala zetu?

SASA LINACHAPISHWA KATIKA LUGHA 182: Afrikaans, Albanian, Amharic, Arabic, Armenian, Armenian (West), Aymara, Azerbaijani, Azerbaijani (Cyrillic), Baoulé, Bengali, Bicol, Bislama, Bulgarian, Cambodian, Cebuano, Chichewa, Chinese (cha Kitamaduni)^o (limerekodiwa katika Kimandarini pekee), Chinese (Sahili), Chitonga, Chuuksese, Cibemba, Croatian, Czech,^o Danish,^o Dutch,^o Efik, English^o (pia Braille), Estonian, Ewe, Fijian, Finnish,^o French,^o Ga, Georgian, German,^o Greek, Greenlandic, Guarani, Gujarati, Gun, Haitian Creole, Hausa, Hebrew, Hiligaynon, Hindi, Hiri Motu, Hungarian,^o Icelandic, Igbo, Iloko, Indonesian, Isoko, Italian,^o Japanese,^o Kannada, Kaonde, Kazakh, Kikongo, Kiluba, Kinyarwanda, Kirghiz, Kiribati,

Kirundi, Kongo, Korean,^o Kwangali, Kwanyama, Latvian, Lingala, Lithuanian, Luganda, Lunda, Luo, Luvale, Macedonian, Malagasy, Malayalam, Maltese, Marathi, Marshallese, Mauritian Creole, Maya, Mizo, Moore, Myanmar, Ndebele, Ndonga, Nepali, Niuean, Norwegian,^o Nyaneka, Oromo, Ossetian, Otetela, Palauan, Pangasinan, Papiamentu (Curaçao), Persian, Polish,^o Ponapean, Portuguese,^o Punjabi, Quechua (Ancash), Quechua (Ayacucho), Quechua (Bolivia), Quechua (Cuzco), Quichua, Rarotongan, Romanian, Russian,^o Samoan, Sango, Sepedi, Serbian, Serbian (Roman), Sesotho, Seychelles Creole, Shona, Silozi, Sinhala, Slovak, Slovenian, Solomon Islands Pidgin, Spanish,^o Sranantongo, Swahili, Swati, Swedish,^o Tagalog,

Tahitian, Tamil, Tatar, Telugu, Tetum, Thai, Tigrinya, Tiv, Tok Pisin, Tongan, Totonac, Tshiluba, Tsonga, Tswana, Tumbuka, Turkish, Tuvaluan, Twi, Tzotzil, Ukrainian, Umbundu, Urdu, Uruund, Uzbek, Venda, Vietnamese, Wallisian, Waray-Waray, Wolaita, Xhosa, Yapese, Yoruba, Zande, Zapotec (Isthmus), Zulu

^o CD zapatikana pia.

^o MP3 CD-ROM zapatikana pia.

^o Magazeti yaliyorekodiwa yanapatikana katika www.jw.org.

3

SALA

Tusali Jinsi Gani?

KUHUSIANA na sala, mapokeo mengi ya kidini yanakazia mambo kama vile jinsi ya kukaa unaposali, maneno yanayotumiwa, na taratibu fulani za kidini. Hata hivyo, Biblia inatusaidia kutokazia fikira mambo hayo na badala yake kufikiria kwa uzito swali hili, “Tunapaswa kusali *jinsi* gani?”

Biblia inasema kwamba watumishi waaminifu wa Mungu walisali wakiwa mahali tofauti-tofauti na katika mkao tofauti. Walisali kimyakimya au kwa sauti ikitegemea hali. Walisali wakiangalia juu mbinguni au wakiwa wamesujudu. Badala ya kutumia sanamu, rozari, au vitabu vya sala, walisali kutoka moyoni kwa maneno yao wenyewe. Ni nini kilichofanya sala zao zisikilizwe na Mungu?

Kama ilivyoelezwa katika makala iliyotangulia, walielekeza sala zao kwa Mungu mmoja tu, Yehova. Kuna jambo lingine muhimu. Tunasoma hivi katika 1 Yohana 5:14: “Huu ndio uhakika ambao tunao kwake, kwamba, hata tukiomba nini *kulingana na mapenzi yake*, yeye hutusikia.” Sala zetu zinapaswa kupatana na mapenzi ya Mungu. Hilo linamaanisha nini?


Ili kusali kulingana na mapenzi ya Mungu, tunahitaji kujua mapenzi yake ni nini. Kwa hiyo, kujifunza Biblia ni muhimu ili kuboresha sala zetu. Je, hilo linamaanisha kwamba ili Mungu asikilize sala

zetu ni lazima tuwe wasomi wa Biblia? Hapana. Lakini Mungu anatazamia tujifunze mapenzi yake na tujitahidi kuyaelewa, na kuishi kupatana na yale tunayojifunza. (Mathayo 7:21-23) Tunahitaji kusali kulingana na yale tunayojifunza.

Kadiri tunavyojifunza kumhusu Yehova na mapenzi yake, ndivyo imani yetu inavyozidi kummaa. Hilo ni jambo lingine muhimu linaloweza kutusaidia kuboresha sala zetu. Yesu alisema: “Mambo yote mnayoomba katika sala, *mkiwa na imani*, mtapokea.” (Mathayo 21:22) Kuwa na imani hakumaanishi kuamini lolote bila kufikiri. Badala yake, kunamaanisha kuamini jambo fulani ambalo hata ingawa halionekani, kuna uthibitisho ulio wazi unaounga mkono jambo hilo. (Waebrania 11:1) Biblia ina uthibitisho mwingi unaoonyesha kwamba Yehova ambaye hatuwezi kumwona ni halisi, anategemeka, na yuko tayari kujibu sala za wale wanaomwamini. Zaidi ya hayo, nyakati zote tunaweza kuomba tuongezewe imani, na Yehova anapenda kutupa kile tunachohitaji.—Luka 17:5; Yakobo 1:17.

Ona pendekezo lingine muhimu kuhusu jinsi ya kusali. Yesu alisema: “Hakuna anayekuja kwa Baba ila kupitia kwangu.” (Yohana 14:6) Kwa hiyo,

Sala ambazo Mungu anasikiliza ni zile zinazopatana na mapenzi yake, zinazotolewa kwa imani, na katika jina la Yesu



Yesu ndiye njia ambayo tunaweza kuitumia kumfikia Baba, Yehova. Hivyo, Yesu aliwaambia wafuasi wake wasali katika jina lake. (Yohana 14:13; 15:16) Hilo halimaanishi kuwa tunapaswa kusali kwa Yesu. Badala yake, tunasali *katika jina la* Yesu, tukikumbuka kwamba tunaweza tu kumfikia Baba yetu mkamilifu na mtakatifu kwa sababu ya Yesu.

Wafuasi wa karibu wa Yesu walimsihi hivi: “Bwana, tufundishe jinsi ya kusali.” (Luka 11:1) Bila shaka, kama ambavyo tumeona, hawakuwa wakioimba wafundishwe mambo ya msingi tu. Badala yake walitaka kujua mengi—kwa maneno mengine walikuwa wakiuliza, “Tunapaswa kusali kuhusu nini?”

4

SALA

Tusali Kuhusu Nini?

IMETAJWA kuwa sala inayorudiwa-rudiwa sana kati ya sala zote za Wakristo. Iwe hilo ni kweli au si kweli, sala ya kielelezo ya Yesu, ambayo nyakati nyingine inaitwa Sala ya Bwana au ya Baba Yetu, ndiyo sala ambayo wengi hawaiielewi. Watu wengi huirudia-rudia kila siku. Lakini Yesu hakukusudia sala hiyo itumiwe kwa njia hiyo. Kwa nini tunasema hivyo?

Muda mfupi tu kabla ya kufundisha sala hiyo,

Yesu alisema: “Mnaposali, msiseme mambo yaleyale tena na tena.” (Mathayo 6:7) Je, Yesu alikuwa akipinga maneno yake mwenyewe kwa kufundisha sala ambayo ingekaririwa na kurudiwa-rudiwa? Bila shaka, hapana! Badala yake, Yesu alikuwa akitufundisha mambo tunayopaswa kutaja na kuyatanguliza tunaposali. Acheni tuchunguze kwa makini yale aliyosema katika sala hiyo iliyoandikwa katika Mathayo 6:9-13.

“Baba yetu uliye mbinguni, jina lako na litakaswe.”

Hivyo, Yesu alikuwa akiwakumbusha wafuasi wake kuwa sala zote zinapaswa kuelekezwa kwa Baba yake, Yehova. Lakini unajua ni kwa nini jina la Mungu ni la maana sana na kwa nini linapaswa kutakaswa, au kufanywa takatifu?

Tangu mwanzo wa historia ya mwanadamu, mambo mengi ya uwongo yamesemwa kuhusu jina takatifu la Mungu. Adui ya Mungu, Shetani, alimwita Yehova Mtawala mwongo na mwenye ubinafsi ambaye hana haki ya kuutawala uumbaji Wake. (Mwanzo 3:1-6) Wengi wameunga mkono madai ya Shetani, wakifundisha kwamba Mungu hana upendo na hana huruma. Pia wanakana kwamba kuna Muumba. Wengine wamelishambulia jina la Mungu, Yehova, kwa kuliondoa katika tafsiri fulani za Biblia na kuwakataza watu wasilitumie.

Biblia inaonyesha kwamba Mungu atarekebisha ukosefu huo wote wa haki. (Ezekieli 39:7) Kwa kufanya hivyo, atatimiza mahitaji yako yote na kutatua matatizo yako. Atafanya hivyo jinsi gani? Maneno yanayofuata katika sala ya Yesu yanatoa jibu.

“Ufalme wako na uje.”

Leo, viongozi wa kidini wamechanganyikiwa sana kuhusiana na Ufalme wa Mungu. Hata hivyo, kama wasikilizaji wa Yesu walivyojua, manabii wa Mungu walikuwa wametabiri tangu zamani kwamba Masihi, Mkombozi aliyechaguliwa na Mungu, angetawala katika Ufalme ambao ungebadili ulimwengu. (Isaya 9:6, 7; Danieli 2:44) Ufalme huo utataka



jina la Mungu kwa kufunua uwongo wa Shetani na kisha kumwondoa Shetani na kazi zake zote. Utaondoa vita, magonjwa, njaa, na hata kifo. (Zaburi 46:9; 72:12-16; Isaya 25:8; 33:24) Unaposali Ufalme wa Mungu uje, unasali kwamba ahadi hizo zote zitimie.

“Mapenzi yako na yatendeke duniani kama ilivyo mbinguni.”

Maneno ya Yesu yanaonyesha kwamba mapenzi ya Mungu yatatimizwa hapa dunia-ni kama yanavyotimizwa mbinguni, makao ya Mungu. Imethibitika kwamba mapenzi ya Mungu hayawezi kuzuiwa yasitimizwe mbinguni; huko, Mwana wa Mungu alipigana vita na Shetani na malaika zake, na kuwatupa hapa duniani. (Ufunuo 12:9-12) Ombi hili la tatu, kama tu yale maombi mawili ya kwanza katika sala ya kielelezo, linatusaidia kukazia uangalifu wetu jambo lililo muhimu hata zaidi, yaani, mapenzi ya Mungu, bali si mapenzi yetu. Ni kutimizwa kwa mapenzi ya Mungu tu ndiko kunakoweza kuwaletea viumbe wake wote mambo mema. Hivyo, hata mwanadamu mkamilifu Yesu alimwambia Baba yake: “Acha, si mapenzi yangu, bali yako yatendeke.”—Luka 22:42.

“Utupe leo mkate wetu kwa ajili ya siku hii.”

Pia, Yesu alionyesha kwamba tunaweza kusali kuhusu mahitaji yetu. Hakuna ubaya wowote kusali kwa Mungu kuhusu mahitaji yetu ya kila siku. Kwa kweli, kufanya hivyo kunatukumbusha kwamba Yehova ndiye “huwapa watu wote uhai na pumzi na vitu vyote.” (Matendo 17:25) Biblia inafunua kwamba yeye ni mzazi mwenye upendo ambaye hufurahia kuwapa watoto wake kile wanachohitaji. Hata hivyo, kama mzazi mwenye upendo, Mungu hawezi kuwapa watu wake vitu ambavyo havitawaletea faida yoyote.

“Utusamehe madeni yetu.”

Je, kweli kuna deni lolote ambalo Mungu anakudai? Je, kweli unahitaji akusamehe deni hilo? Watu wengi leo hawaelewi dhambi ni nini wala hawaelewi uzito wake. Laki-ni Biblia inafundisha kwamba dhambi ndiyo chanzo cha matatizo yetu, kwa sababu ndiyo inayosababisha kifo cha wanadamu. Kwa kuwa tumezaliwa katika dhambi, mara kwa mara sote tunatenda dhambi, na tunategemea msamaha wa Mungu ili tuweze kuisi milele wakati ujao. (Waroma 3:23; 5:12; 6:23) Inatuliza kujua maneno haya ya Biblia: “Wewe, Ee Yehova, ni mwema na uko tayari kusamehe.”—Zaburi 86:5.

“Utukomboe kutokana na yule mwovu.”

Je, unajua ni kwa nini unahitaji sana ulinzi wa Mungu? Wengi hawataki kuamini kwamba Shetani, “yule mwovu,” yupo. Lakini Yesu alifundisha kwamba Shetani ni kiumbe halisi, hata akamwita “mtawala wa ulimwengu huu.” (Yohana 12:31; 16:11) Shetani ameupotosha ulimwengu huu anaoutawala, na anatamani sana kukupotosha ili usiweze kusitawisha uhusiano wa karibu pamoja na Baba yako, Yehova. (1 Petro 5:8) Hata hivyo, Yehova ana nguvu zaidi kuliko Shetani na anafurahia kuwalinda wale wanaompenda.

Bila shaka, mambo ambayo tumezungumzia katika sala ya kielelezo ya Yesu, hayatii ndani kila jambo linalopaswa kutajwa katika sala. Kumbuka andiko la 1 Yohana 5:14 linatuambia hivi kumhusu Mungu: “Hata tukiomba *nini* kulingana na mapenzi yake, yeye hutusikia.” Hivyo, usifiki-

ri kwamba mahangaiko yako ni madogo sana hivi kwamba hupaswi kumweleza Mungu katika sala.—1 Petro 5:7.

Hata hivyo, namna gani kuhusu mahali na wakati wa kusali? Je, ni muhimu kufikiria mambo haya?

Tusali Wakati Gani na Mahali Gani?

BILA shaka, umeona kwamba dini nyingi kubwa zinakazia kuwa na majengo ya sala yenye madoi-do na zinapanga wakati hususa wa kusali. Je, Biblia inasema ni lazima tuwe na mahali hususa na wakati hususa wa kusali?

Biblia inaonyesha kwamba kuna nyakati zinazofaa za kusali. Kwa mfano, kabla ya kula na wafuasi wake, Yesu alitoa sala ya kumshukuru Mungu. (Luka 22:17) Na wanafunzi wake walipokutana ili kuabudu, walisali pamoja. Hivyo, walieleza desturi iliyokuwa ikifuatwa tangu zamani katika masinagogi ya Wayahudi na katika hekalu huko Yerusalemu. Mungu alikusudia hekalu liwe “nyumba ya sala kwa ajili ya mataifa yote.”—Marko 11:17.

Watumishi wa Mungu wanapokusanyika na kusali pamoja, maombi yao yanaweza kuwa na

matokeo mazuri. Mungu hufurahi ikiwa wanakusanyika wakiwa na nia moja na sala inayotolewa kwa ajili yao inapatana na kanuni za Maandiko. Sala hiyo hata inaweza kumchochea mtu afanye jambo ambalo huenda hangefanya. (Waebrania 13:18, 19) Mashahidi wa Yehova husali kwa ukawaida katika mikutano yao. Unakaribishwa kwa uchangamfu uende kwenye Jumba la Ufalme ambalo liko karibu nawe ili usikie sala hizo.

Hata hivyo, Biblia haisemi ni lazima tuwe na mahali hususa na wakati hususa wa kusali. Katika Biblia, tunasoma kuhusu watumishi wa Mungu waliosali wakati na mahali tofauti-tofauti. Yesu alisema: “Unaposali, ingia ndani ya chumba chako cha faragha na, baada ya kufunga mlango wako, sali kwa Baba yako aliye mahali pa siri; ndipo Baba yako anayetazama akiwa mahali pa siri atakulipa.”—Mathayo 6:6.

Bila shaka, huo ni mwaliko wenye kupendeza, sivyo? Unaweza kusali kwa Mwenye Enzi Kuu ya ulimwengu wote wakati wowote, hata ukiwa faraghani, na kuwa na hakika kwamba atakusikiliza. Si ajabu kwamba mara nyingi Yesu alihitaji kuwa peke yake ili asali! Wakati fulani alisali kwa Mungu usiku kucha, bila shaka, akitafuta mwongozo wa kufanya uamuzi fulani mzito.—Luka 6:12, 13.

Wanaume na wanawake wengine katika Biblia walisali walipotaka kufanya maamuzi mazito au walipopatwa na hali fulani ngumu. Nyakati fulani walisali kwa sauti na nyakati nyingine wakasali kimyakimya; walisali walipokuwa katika kikundi na hata walipokuwa peke yao. Jambo muhimu ni kwamba walisali. Hata Mungu huwaambia watumishi wake hivi: “Salini bila kuacha.” (1 Wathesalonike 5:17) Yuko tayari kuwasikiliza bila kuchoka wale wanaofanya mapenzi yake. Je, huo si mwaliko wenye upendo?

Bila shaka, katika ulimwengu huu wenye shaka, wengi wanataka kujua ikiwa sala inaweza kuwasaidia. Huenda ukauliza, ‘Je, kweli sala inaweza kunisaidia?’

Tunaweza kusali wakati wowote, mahali popote



Je, Inaweza Kutusaidia?

JE, SALA inaweza kutusaidia? Jibu ni ndiyo, kwa kuwa Biblia inaonyesha kwamba sala za watumishi waaminifu wa Mungu zinawanufaisha. (Luka 22:40; Yakobo 5:13) Kwa kweli, sala inaweza kutusaidia sana kiroho, kihisia, au hata kimwili. Jinsi gani?

Tuseme kwamba mtoto wako amepokea zawadi. Je, ungemfundisha kwamba inatosha tu *kuhisi* shukrani moyoni? Au ungemfundisha *kusema* asante? Tunapoeleza hisia zetu muhimu, tunafanya ziwe wazi na hata ziwe na uzito zaidi. Je, inaweza kuwa hivyo tunapozungumza na Mungu? Bila shaka! Fikiria mifano fulani.

Sala za shukrani. Tunapomshukuru Baba yetu kwa mambo mazuri anayotufanyia, tunaonyesha kwamba tunathamini baraka hizo. Kwa hiyo, tunaweza kujihisi wenye shukrani zaidi, wenye furaha zaidi, na wenye mtazamo mzuri hata zaidi. —Wafilipi 4:6.

Mfano: Yesu alimshukuru Baba yake kwa jinsi alivyosikiliza na kujibu sala zake.—Yohana 11:41.

Sala za kuomba msamaha. Tunapomwomba Mungu msamaha tunafanya dhamiri yetu iwe yenye nguvu, toba yetu iwe ya kutoka moyoni, na tunaelewa zaidi uzito wa dhambi. Pia, tunapata kitulizo kutokana na hali yenye kulemea ya kujisikia kuwa wenye hatia.

Mfano: Daudi alisali ili kuonyesha toba na huzuni yake.—Zaburi 51.

Sala za kuomba mwongozo na hekima. Tunapomwomba Yehova atuongoze au atupe hekima ili

tufanye maamuzi yanayofaa, jambo hilo linaweza kutusaidia kuwa wanyenyekevu. Pia, linaweza kutukumbusha kwamba tumepungukiwa na vilevile kutusaidia kuimarisha imani kwa Baba yetu wa mbinguni.—Methali 3:5, 6.

Mfano: Kwa unyenyekevu Sulemani aliomba mwongozo na hekima ili aweze kutawala Israeli.—1 Wafalme 3:5-12.

Sala wakati wa taabu. Tunapomweleza Yehova yaliyo moyoni mwetu wakati ambapo tumevurugika kihisia, mioyo yetu inaburudika na tunajifunza kumtegemea badala ya kujitegemea wenyewe.—Zaburi 62:8.

Mfano: Mfalme Asa alisali alipokabili adui hatari.—2 Mambo ya Nyakati 14:11.

Sala za kuwatakia hali njema wenye uhitaji. Sala kama hizo hutuwezesha kushinda ubinafsi na kuwa wenye rehema na huruma.


Mfano: Yesu alisali kwa ajili ya wafuasi wake.—Yohana 17:9-17.

Sala za sifa. Tunapomtukuza Yehova kwa ajili ya kazi na sifa zake za ajabu, heshima na uthamini wetu kwake unaongezeka. Sala kama hizo zinaweza kutusaidia kumkaribia Mungu ambaye pia ni Baba yetu.

Mfano: Daudi alimsifu Mungu kwa uchangamfu kwa sababu ya kazi zake za uumbaji.—Zaburi 8.

Baraka nyingine inayohusianishwa na sala ni “amani ya Mungu yenye ubora unaozidi fikira zote.” (Wafilipi 4:7) Si rahisi kupata utulivu katika ulimwengu huu wenye msukosuko. Lakin kuwa na utulivu kunatusaidia kuwa na afya nzuri. (Methali 14:30) Hata hivyo, je, utulivu huo unatokana tu na jitihada zetu wenyewe? Au kuna jambo lingine muhimu linalohusika?

Sala ina manufaa mengi—kimwili, kihisia, na hata kiroho



Je, Mungu Atasikiliza na Kujibu Sala Zetu?

SWALI hilo linafanya watu wasisimuke na kuwa na hamu ya kupata jibu. Biblia inaonyesha kwamba Yehova *husikiliza* sala leo. Iwe atasikiliza sala za mtu au hatazisikiliza, hilo hasa litategemea mtu mwenyewe.

Yesu aliwalaumu viongozi wa kidini wa nyakati zake ambao walisalizi kwa unafiki, wakihangai- kua tu kuonekana kuwa waadilifu. Alisema kuwa watu hao wangepata “thawabu yao kwa ukamili,” akimaanisha kwamba wangepata tu kile walichotaka sana, yaani, kuonekana na watu, bali si kile walichohitaji, yaani, kusikilizwa na Mungu. (Mathayo 6:5) Vivyo hivyo leo, wengi husali kulingana na mapenzi yao bali si ya Mungu. Kwa kuwa wanapuuza kanuni za Biblia ambazo tumezungumzia, Mungu hasikilizi sala zao.

Namna gani wewe? Je, Mungu atasikiliza na kujibu sala zako? Jibu halitegemei wewe ni wa jamii, taifa, au cheo gani katika jamii. Biblia inatuhakikishia hivi: “Mungu hana ubaguzi, bali katika kila taifa mtu ambaye anamwogopa na kutenda uadilifu anakubalika kwake.” (Matendo 10:34, 35) Je, wewe unafanya hivyo? Ikiwa unamwogopa Mungu, inamaanisha kwamba unamheshimu sana, na hutaki kumchukiza. Unapotenda uadilifu, unajitahidi kufanya yale ambayo Mungu anasema ni sawa badala ya kufanya mapenzi yako au ya wanadamu wenzako. Je, kweli unataka Mungu asikilize sala zako? Biblia inaonyesha jinsi unavyoweza kusali ili Mungu asikilize sala zako.*

Bila shaka, wengi wanataka Mungu ajibu sala zao kwa kufanya muujiza. Lakini hata katika nyakati za Biblia, si mara nyingi Mungu alijibu sala

kwa kufanya muujiza. Baada ya muujiza mmoja kufanywa, miaka mingi ilipita kabla ya mwingine kufanywa. Zaidi ya hilo, Biblia inaonyesha kwamba kipindi cha kufanya muujiza kiliisha baada ya siku za mitume. (1 Wakorintho 13:8-10) Je, hilo linamaanisha kwamba leo Mungu hajibu sala? Hapana! Ona baadhi ya sala ambazo anajibu.

Mungu anatupa hekima. Yehova ndiye Chanzo pekee cha hekima yote ya kweli. Yeye huitoa kwa ukarimu, akiwapa wale wanaotaka mwongozo wake na wanaojitahidi kuishi kulingana na mwongozo huo.—Yakobo 1:5.

Mungu hutupa roho yake takatifu na faida zote zinazotokana nayo. Roho takatifu ni nguvu ya utendaji ya Mungu. Hakuna nguvu inayozidi hiyo. Inaweza kutusaidia kuvumilia majaribu. Inaweza kutupa amani tunapokabili hali ngumu. Inaweza kutusaidia kusitawisha sifa nyingine nzuri na zinazopendeza. (Wagalatia 5:22, 23) Yesu aliwahakikishia wafuasi wake kwamba Mungu hutoa zawadi hiyo kwa ukarimu.—Luka 11:13.

Mungu huwapa ujuzi wale wanaomtafuta kwa bidii. (Matendo 17:26, 27) Ulimwenguni pote, kuna watu ambao wanatafuta kweli kwa unyofu. Wanataka kujua kumhusu Mungu—jina lake ni nani, kusudi lake la kuumba dunia na wanadamu, na jinsi wanavyoweza kumkaribia. (Yakobo 4:8) Mara nyingi, Mashahidi wa Yehova wanakutana na watu kama hao, nao hufurahi kujibu maswali hayo kwa kutumia Biblia.

Je, hiyo ndiyo sababu ulichukua gazeti hili? Je, unamtafuta Mungu? Labda hii ndiyo njia anayotumia kujibu sala yako.

* Kwa habari zaidi kuhusu jinsi ya kusali na kusikiliza na Mungu, ona sura ya 17 ya kitabu *Biblia Inafundisha Nini Hasa?* kilichochapishwa na Mashahidi wa Yehova.



JE, WAJUA?

Kwa nini kitabu cha Kwanza cha Wakorintho kinazungumza kuhusu nyama iliyotolewa dhabihu kwa sanamu?

■ Mtume Paulo aliandika: “Endeleeni kula kila kitu kinachouzwa katika soko la nyama, bila kuchunguza kwa sababu ya dhamiri yenu.” (1 Wakorintho 10:25) Nyama hizo zilitoka wapi?

Dhabihu za wanyama zilikuwa sehemu muhimu ya sherehe katika mahekalu ya Wagiriki na Waroma, lakini nyama yote iliyotolewa dhabihu haikuliwa wakati wa sherehe. Hivyo, nyama iliyobaki kwenye mahekalu hayo ya kipagani iliuzwa sokoni. Kitabu kimoja (*Idol Meat in Corinth*) kinasema: “Viongozi wa madhehebu . . . nyakati nyingine wanaitwa wapishi na/au wachinjaji. Nyama walipopewa kama malipo kwa kuchinja mnyama aliyetolewa dhabihu, waliuza sokoni.”

Kwa hiyo, si nyama zote zilizouzwa sokoni ambazo zilikuwa mabaki ya nyama zilizotumiwa katika sherehe za kidini. Kwa kuwa, viunzi vizima vya mifupa ya kondoo vilichimbuliwa katika eneo la soko la nyama (Kilatini, *macellum*) la Pompeii. Msofiri Henry J. Cadbury anasema jambo hilo linadokeza kwamba “huenda nyama zilizouzwa ni za wanyama hai au wanyama waliochinjwa kwenye *macellum* na pia nyama za wanyama waliochinjwa au kutolewa dhabihu hekaluni.”

Paulo alikuwa akitoa hoja kwamba ingawa Wakristo hawangeshiriki katika ibada ya kipagani, kimsingi nyama iliyotolewa dhabihu hekaluni haikuwa imetiwa unajisi.



SAHANI YA UDONGO ILIYO NA PICHA YA WATU WAKITOA DHABIHU YA WANYAMA KATIKA KARNE YA SITA K.W.K. Musée du Louvre, Paris

Kwa nini kulikuwa na utengano kati ya Wayahudi na Wasamaria wa siku za Yesu?

■ Andiko la Yohana 4:9 linasema kuwa ‘Wayahudi hawakuwa na shughuli na Wasamaria.’ Yaonekana utengano huo ulianza wakati Yeroboamu alipoanzisha ibada ya sanamu katika ufalme wa kaskazini wa makabila kumi ya Israeli. (1 Wafalme 12:26-30) Wasamaria walikuwa wakaaji wa Samaria, jiji kuu la ufalme wa kaskazini. Baadaye wakaaji wote wa ufalme wa kaskazini walii-twa Wasamaria. Waashuru walipoteka makabila kumi ya ufalme huo mwaka wa 740 K.W.K., walileta wapagani kutoka nchi nyingine wawe wakaaji wa eneo lote la ufalme wa kaskazini. Watu hao walioana na Wasamaria na hivyo ibada ya Wasamaria ikapotoshwa hata zaidi.

Karne nyingi baadaye, Wasamaria walipinga juhudi za Wayahudi waliorudi kutoka uhamishoni Babiloni za kuje-nga hekalu la Yehova na kuta za jiji la Yerusalemu. (Ezra 4:1-23; Nehemia 4:1-8) Ushindani wa kidini uliongezeka wakati Wasamaria walipojenga hekalu lao wenyewe kwenye Mlima Gerizimu, yapata karne ya nne K.W.K.

Siku za Yesu neno “Msamaria” lilihusianishwa zaidi na dini kuliko eneo, na lilitumiwa kurejelea mshiriki wa madhehebu iliyokuwa imeenea sana Samaria. Wasamaria bado waliabudu kwenye Mlima Gerizimu, na Wayahudi waliwadharau sana.—Yohana 4:20-22; 8:48.



YEROBOAMU ALIANZISHA IBADA YA SANAMU

Je, Mashahidi wa Yehova wanaponya kimuujiza?

■ Mashahidi wa Yehova hawajawahi kuponya watu kimuujiza. Kama Yesu, wanaamini kwamba kazi yao kuu ni kuhubiri habari njema kuhusu Ufalme wa Mungu. Pia wanaamini kwamba Wakristo wa kweli wanatambuliwa si kwa kuponya kimuujiza, bali kwa jambo fulani ambalo ni muhimu zaidi.

Ni kweli kwamba uponyaji ambao Yesu Kristo alichochewa na huruma kuufanya katika karne ya kwanza, ni muhimu sana kwetu. Kwa kufanya hivyo, alitoa uhakikisho kamili kuwa chini ya utawala wake akiwa Mfalme wa Ufalme wa Mungu, “haku-na mkaaji atakayesema: ‘Mimi ni mgonjwa.’”—Isaya 33:24.

Namna gani leo? Watu wa dini zinazodai kuwa za Kikristo na dini nyinginezo, wamedai kwamba wanaweza kuwaponya watu kimuujiza. Hata hivyo, Yesu alitoa onyo kali kuhusu watu ambao wangedai kuwa ‘wamefanya miujiza mingi’ katika jina lake. Angewaambia: “Sikuwajua nyinyi kamwe; ondokeni mbele yangu, enyi watenda maovu.” (Mathayo 7:22, 23, *Biblia Habari Njema*) Kwa hivyo, je, kweli uponyaji wa kimuujiza unaodaiwa kufanywa leo unathibitisha kwamba mtu amekubaliwa au kubarikiwa na Mungu?

Ona vile Biblia inavyosema kuhusu uponyaji uliofanywa na Yesu. Tunapolinganisha jinsi Yesu alivyoponya na jinsi waponyaji wa siku hizi wanavyofanya, tunaweza kuamua urahisi kama uponyaji wa siku hizi unatoka kwa Mungu.

Yesu hakutumia uwezo wa kuponya kama njia ya kupata wafuasi au kuvuta umati uje kumsikiliza. Kinyume cha hilo, aliponya watu fulani bila kujionyesha waziwazi. Mara nyingi aliwambia wale aliwaponya wasimwambie mtu yeyote kuhusu muujiza huo.—Luka 5:13, 14.

Yesu hakuwaomba watu aliwaponya watoe pesa. (Mathayo 10:8) Pia, hakushindwa kumponya mtu

Je, kweli wale wanaodai kuponya kimuujiza siku hizi (picha upande wa kulia) wanaungwa mkono na Mungu?

yeyote. Wagonjwa wote waliokuja kwake waliponywa kabisa, na uponyaji huo haukutegemea imani ya mtu. (Luka 6:19; Yohana 5:5-9, 13) Yesu hata aliwafufua wafu!—Luka 7:11-17; 8:40-56; Yohana 11:38-44.

Ingawa Yesu alifanya miujiza hiyo ya kuponya, jambo lililokuwa muhimu katika huduma yake halikuwa kuwakusanya watu kwa kuwageuza imani kupitia matendo ya kimuujiza yenye kuchochea hisia. Badala yake, kazi yake muhimu ilikuwa kutangaza habari njema ya Ufalme wa Mungu. Yesu aliwatarisha wafuasi wake kwa ajili ya kazi ya kufanya wanafunzi, nao wangewafundisha wengine kuhusu tumaini la kupata afya kamilifu chini ya Ufalme wa Mungu.—Mathayo 28:19, 20.

Ni kweli kwamba baadhi ya wafuasi wa Yesu wa karne ya kwanza walipewa zawadi za kipekee za kuponya, lakini zawadi hizo zingefikia mwisho. (1 Wakorintho 12:29, 30; 13:8, 13) Wakristo wa kweli leo wanatambuliwa, si kupitia kuponya kimuujiza, bali kupitia upendo wa kujidhabihu unaowaunganisha. (Yohana 13:35) Kuponya kimuujiza leo hakujatokea familia ya Wakristo kutoka malezi na jamii tofauti-tofauti ambao wanaunganishwa pamoja na upendo.

Hata hivyo, kuna Wakristo ambao wanaunganishwa na kifungo cha upendo. Kifungo hicho kina nguvu sana hivi kwamba wanakataa kuumizana—au kumuumiza mtu mwingine—hata wakati wa vita vikali vya wanadamu. Ni nani hao? Mashahidi wa Yehova. Duniani kote, wanajulikana kwa kuonyesha upendo kama wa Kristo. Kuwaunganisha watu wa jamii, mataifa, utamaduni, na makabila mbalimbali ni muujiza wa aina fulani, na jambo hilo linawezekana kupitia tu roho takatifu ya Mungu. Unaalikwa uhudhurie mmoja kati ya mikutano yao na ujionee mwenyewe.





IGENI IMANI YAO

'Aliendelea Kukua Akiwa na Yehova'

SAMWELI aliwatazama watu wake. Taifa lilikuwa limekusanyika katika mji wa Gilgali, baada ya kuitwa na mtumishi huyo mwaminifu ambaye alikuwa ametumika akiwa nabii na mwamuzi kwa muda mrefu. Ilikuwa kati ya mwezi wa Mei (Mwezi wa 5) au Juni (Mwezi wa 6) kulingana na kalenda ya wakati wetu, nayo majira ya kiangazi yalikuwa yameanza. Mashamba katika eneo hilo yalikuwa yamejaa ngano iliyokuwa tayari kuvunwa. Umati uliokuwa umekusanyika ulinyamaza. Samweli angeweza kufikia mioyo yao jinsi gani?

Watu hawakuelewa uzito wa hali iliyowakabili. Walikuwa wamesisitiza kuwa na mfalme wa kibinadamu. Hawakujua kwamba walikuwa wanaonyesha ukosefu mkubwa wa heshima kwa Mungu wao, Yehova, na kwa nabii wake pia. Kwa kweli, walikuwa wanamkataa Yehova kuwa Mfalme wao! Samweli angewasaidia jinsi gani watubu?

Samweli alizungumza nao akisema: "Mimi ni-mezeeka nami nina mvi." Nywele zake nyeupe zilifanya maneno yake yawe na uzito zaidi. Kisha akasema: "Nimetembea mbele yenu tangu ujana wangu mpaka leo hii." (1 Samweli 11:14, 15; 12:2) Ingawa Samweli alikuwa amezeeka hakuwa amesahau siku za ujana wake. Bado alikuwa anakumbuka siku hizo. Maamuzi aliyofanya wakati huo akiwa kijana, yalifanya awe na imani na kujitoa kwa Mungu wake, Yehova, katika maisha yake.

Samweli alihitaji kuendelea kusitawisha na kudumisha imani yake, ingawa alizungukwa na watu waliokosa imani na wasio waaminifu. Hata leo, si rahisi kusitawisha imani, kwa kuwa tunaiishi katika ulimwengu usio na imani na uliopotoka. Hebu tuone mambo tunayoweza kujifunza kutokana na mfano wa Samweli, kuanzia wakati alipokuwa mvulana mdogo.

'Alihudumu Mbele za Yehova Akiwa Mvulana'

Maisha ya utotoni ya Samweli hayakuwa ya kawaida. Muda mfupi baada ya kuachishwa kunyoo

nya, labda akiwa na miaka minne hivi, alianza kutumika katika maskani au hema la kukutania la Yehova huko Shilo, lilokuwa umbali wa zaidi ya kilomita 30 kutoka nyumbani kwao, Rama. Wazazi wake Elkana na Hana, walimweka wakfu kwa Yehova kwa ajili ya utumishi wa pekee na hivyo kumfanya kuwa Mnadhiri katika maisha yake yote.* Je, hilo lilimaanisha kuwa wazazi wa Samweli hawakumpenda wala hawakutaka kumtunza?

Hapana! Walijua kuwa mwana wao angetunzwa huko Shilo. Bila shaka, Kuhani Mkuu Eli alihakikisha kwamba Samweli ametunzwa vizuri kwa kuwa alifanya kazi karibu naye. Pia, kulikuwa na wanawake kadhaa waliofanya kazi fulani katika hema la kukutania, na yaelekea walifanya kazi hiyo kwa utaratibu.—Kutoka 38:8.

Zaidi ya hayo, Hana na Elkana hawakumsahau mtoto wao wa kwanza mpendwa, ambaye kuzaliwa kwake kulitokana na kujibiwa kwa sala ya Hana. Hana alikuwa amemwomba Mungu mtoto wa kiume, na kuahidi kuwa angemtoa ili amtumikie Mungu katika utumishi mtakatifu maisha yake yote. Kila mwaka, Hana alipomtembelea Samweli alimletea koti jipya lisilo na mikono, ambalo angetumia katika utumishi wake katika hema la kukutania. Kwa kweli, kijana huyo mdo-

* Wanadhiri walikuwa chini ya nadhiri iliyowakataza kunywa vileo na kunyoo nywele zao. Wengi wao walikuwa Wanadhiri kwa muda fulani hususa, lakini wachache kati yao kama Samsoni, Samweli, na Yohana Mbatizaji, walikuwa Wanadhiri katika maisha yao yote.

go alifurahi sana mama yake alipomtembelea. Bila shaka, Samweli alifanikiwa kwa sababu wazazi wake wenye upendo walimtia moyo na kumwongoza walipomfundisha kwamba lilikuwa pendeleo kubwa kumtumikia Yehova katika sehemu hiyo ya kipekee.

Leo, wazazi wanaweza kujifunza mengi kutoka kwa Hana na Elkana. Wazazi wanapowalea watoto wao, ni jambo la kawaida kukazia fikira mahitaji ya kimwili huku wakipuuza mahitaji ya kiroho ya watoto hao. Lakini wazazi wa Samweli walitanguliza mambo ya kiroho, na hilo lilichangia sana sifa ambazo mwana wao Samweli angekuwa nazo akiwa mtu mzima.—Methali 22:6.

Alipokuwa akiendelea kukua, unaweza kuwazia kijana huyo akitembea huku na huku kujionea milima iliyozunguka Shilo. Alipotazama mji huo kutoka mlimani na pia kutazama bonde lililokuwa upande mmoja wa mji huo, yaelekea moyo wake ulijawa na furaha hasa alipoona hema la kukutania la Yehova. Kwa kweli, hema hilo lilikuwa ni mahali patakatifu.* Lilikuwa limejengwa miaka 400 hivi iliyopita chini ya mwongozo wa Musa, na lilikuwa mahali pa ibada safi ya Yehova duniani kote.

Kijana Samweli alipenda hema la kukutania. Tunasoma hivi katika simulizi aliloandika baadaye: “Samweli alikuwa akihudumu mbele za Yehova, akiwa mvulana, amejifunga efodi ya kitani.” (1 Samweli 2:18) Koti hilo la kitani linaonyesha wazi kuwa Samweli aliwasaidia makuhani ndani ya hema la kukutania. Ingawa Samweli hakuwa wa jamii ya kikuhanu, alikuwa na majukumu yaliyotia ndani kufungua milango ya ua wa hema la kukutania kila asubuhi na kumsaidia Eli aliyekuwa mzee kwa umri. Samweli alifurahia pendeleo hilo, hata hivyo, baada ya muda alianza kutaabika

* Mahali patakatifu palikuwa ni hema kubwa la kukutania lenye umbo la mstali (*rectangle*), lililoshikiliwa kwa viunzi vya mbao. Hata hivyo, hema hilo lilikuwa limetengezwa kwa vitu bora sana, yaani, ngozi ya sili, vitambaa vilivyopambwa vizuri, na mbao za bei ya juu zilizofunikwa kwa fedha na dhahabu. Mahali hapo patakatifu palizungukwa na ua. Ndani ya ua huo palikuwa pia na madhabahu yenye kupendeza ya kutolea dhabihu. Baadaye, yaelekea vyumba vingine vilivyotumiwa na makuhani vilijengwa kandokando ya hema hilo. Huenda Samweli alilala ndani ya mjawapo ya vyumba hivyo.

moyoni. Kulikuwa na jambo baya sana lililokuwa likiendelea ndani ya nyumba ya Yehova.

Samweli Hakuathiriwa na Upotovu Uliomzunguka

Alipokuwa na umri mdogo, Samweli alijionea upotovu na uovu mkubwa uliofanywa waziwazi. Eli alikuwa na wana wawili, Hofni na Finehasi. Simulizi la Samweli linasema: “Wana wa Eli walikuwa watu wasiofaa kitu; hawakumtambua Yehova.” (1 Samweli 2:12) Mawazo mawili yaliyo katika mstari huo yanapatana. Hofni na Finehasi walikuwa “watu wasiofaa kitu” kwa kuwa hawakumheshimu Yehova. Hawakufikiria kamwe kani na sheria zake za uadilifu. Jambo hilo lilikuwa chanzo kikuu cha dhambi walizotenda.

Sheria ya Mungu ilitaja waziwazi kazi za makuhani na jinsi walivyopaswa kutoa dhabihu katika madhabahu. Mungu alifanya hivyo kwa sababu nzuri! Dhabihu hizo ziliwakilisha mpango wa Mungu wa kusamehe dhambi ili watu wawe safi machoni pake, na kustahili kupata baraka na mwongozo wake. Lakini Hofni na Finehasi waliwaongoza makuhani wenzao kutoheshimu dhambi zilizokuwa zikitolewa.*

Hebu wazia jinsi kijana Samweli alivyotazama uovu huo mkubwa uliokuwa ukiendelea bila kurekebisha. Aliona watu wangapi—kutia ndani watu wapole, maskini, na waliokandamizwa—wakija katika hema takatifu la kukutania huku wakitumaini kufarijiwa na kutiwa moyo, lakini badala yake kuondoka wakiwa wamevunjika moyo, wameumia, au kuaibishwa? Na wazia jinsi alivyohisi alipotambua kuwa Hofni na Finehasi hawakutii sheria za Yehova kuhusu ngono, kwa kuwa

* Simulizi hilo linatoa mifano miwili inayoonyesha jinsi walivyokosa heshima. Kwanza, Sheria ilitaja kihusua vipande vya nyama vilivyotolewa dhabihu ambavyo makuhani waliruhusiwa kula. (Kumbukumbu la Torati 18:3) Lakini katika hema la kukutania, makuhani hao waovu walifanya jambo tofauti kabisa. Waliwalazimisha wahudumu wao kuingiza uma mkubwa ndani ya chungu cha kupikia ambacho kilikuwa na nyama zilizokuwa zikitokota, na kutoa kipande chochote kizuri walichopata! Pia, watu walipoleta dhabihu zao ili ziteketezwe juu ya madhabahu, makuhani hao waovu waliwatuma wahudumu wao kuwasumbua watu waliioleta dhabihu kwa kuwaambia wawape nyama mbichi kabla ya kumtolea Yehova dhabihu ya sehemu ya mafuta.—Mambo ya Walawi 3:3-5; 1 Samweli 2:13-17.

walikuwa na uhusiano wa kingono na wanawake fulani waliokuwa wakitumika katika hema la kukutania? (1 Samweli 2:22) Huenda alitazamia Eli angechukua hatua fulani kuhusu jambo hilo.

Eli alikuwa na uwezo wa kutatua tatizo hilo lililokuwa linazidi kuwa baya. Akiwa kuhani mkuu, alikuwa na jukumu la kusimamia kila kitu kilichokuwa kikitendeka katika hema la kukutania. Pia akiwa baba, alikuwa na jukumu la kuwarekebisha watoto wake. Mambo hayo mabaya yaliwaumiza wao wenyewe na watu wengine wengi katika nchi hiyo. Hata hivyo, Eli alishindwa kutimiza majukumu yake, akiwa baba na akiwa kuhani mkuu. Aliwakaripia watoto wake kwa unyonge tu. (1 Samweli 2:23-25) Lakini watoto wake walihitaji nidhamu kali zaidi. Walikuwa wakitenda dhambi zilizostahili kifo!

Hali hiyo ilizidi kuwa mbaya mpaka Yehova akatuma ujumbe mzito wa hukumu kwa Eli kupitia “mtu wa Mungu,” yaani, nabii fulani ambaye hatajwi jina. Yehova alimwambia Eli hivi: “Unaeendelea kuwaheshimu wana wako kuliko mimi.” Hivyo, Mungu akatabiri kuwa wana waovu wa Eli wangekufa wote wawili siku moja na familia ya Eli ingeteseka sana, na hata kupoteza pendeleo la kuwa makuhani. Je, onyo hilo kali lilileta badiliko lolote katika familia hiyo? Simulizi hilo linaonyesha kwamba familia ya Eli haikubadilika.—1 Samweli 2:27–3:1.

Upotovu huo wote ulimwathiri Samweli jinsi gani? Ingawa hali ilikuwa mbaya, bado simulizi hilo linataja mambo fulani mazuri, yaani, habari njema kuhusu ukuzi na maendeleo ya Samweli. Kumbuka kuwa kitabu cha 1 Samweli 2:18 kinasema kwamba Samweli alikuwa “akihudumu mbele za Yehova, akiwa mvulana.” Hata katika umri huo mchanga, Samweli alitumia maisha yake kumtumikia Mungu. Katika mstari wa 21 tunasoma jambo lingine lenye kutia moyo hata zaidi: ‘Mvulana Samweli aliendelea kukua akiwa na Yehova.’ Kadiri alivyoendelea kukua, ndivyo uhusiano wake na Baba yake wa mbinguni ulivyoimarika. Uhusiano huo wa kibinafsi pamoja na Yehova, ndio ulinzi hakika dhidi ya upotovu wowote.

Ingekuwa rahisi kwa Samweli kusema kwamba ikiwa kuhani mkuu na watoto wake wanaweza ku-

fanya dhambi, hata yeye anaweza kufanya jambo lolote lile alilotaka. Lakini, upotovu unaotendwa na wengine, kutia ndani wale wenye mamlaka, si sababu ya kutenda dhambi. Leo vijana wengi Wakristo wanaiga mfano wa Samweli na ‘kuendelea kukua wakiwa na Yehova’—hata ikiwa watu wanaowazunguka hawawawekei mfano mzuri.

Samweli alifaidika jinsi gani kwa kuishi maisha ya aina hiyo? Tunasoma hivi: “Na wakati huo wote mvulana Samweli alikuwa akiendelea kukua na kupendwa na Yehova na vilevile na wanadamu.” (1 Samweli 2:26) Kwa hiyo, Samweli alipendwa na watu ambao walikuwa na maoni yanayofaa. Yehova mwenyewe alimpenda na kumtunza kijana huyo kwa sababu ya uaminifu wake. Samweli alikuwa na hakika kuwa Mungu angechukua hatua ya kumaliza uovu uliokuwa ukiendelea huko Shilo, lakini huenda alijiuliza Mungu angefanya hivyo wakati gani.

“Sema, kwa Maana Mtumishi Wako Anasikiliza”

Usiku mmoja swali hilo lilijibiwa. Asubuhi ilikuwa inakaribia lakini bado kulikuwa na giza; nuru ya taa kubwa ya hema ilikuwa bado inaangaza. Wakati huo, Samweli akasikia sauti ikiita jina lake. Alifikiri kuwa alikuwa akiitwa na Eli, ambaye wakati huo alikuwa mzee sana na hakuwa anaona vizuri. Samweli aliamka na ‘kukimbia’ kwa mzee huyo. Je, unaweza kuwazia akilini, mvulana huyo akikimbia bila viatu ili kujua Eli alihitaji nini? Inatia moyo sana kuona kwamba Samweli alimheshimu na kumtendea Eli kwa fadhili. Ingawa Eli alikuwa akitenda dhambi, bado alikuwa kuhani mkuu wa Yehova.—1 Samweli 3:2-5.

Samweli alimwamsha Eli na kusema: “Mimi hapa, kwa maana umeniita.” Lakini Eli akasema kwamba hakuwa amemwita na akamwambia arudi kulala. Jambo hilo lilitendeka tena na tena! Mwishowe, Eli akatambua kilichokuwa kikiendelea. Muda ulikuwa umepita tangu Yehova alipotuma maono au ujumbe wa kinabii kwa watu, na haikuwa vigumu kujua ni kwa nini. Lakini Eli alijua kwamba Yehova alikuwa akizungumza tena—wakati huu kupitia Samweli! Eli alimwambia arudi kulala na akamweleza jinsi ya kujibu ataka-

poitwa tena. Samweli alitii. Punde si punde, akasia sauti ikiita: “Samweli, Samweli!” Naye akajibu: “Sema, kwa maana mtumishi wako anasikiliza.” —1 Samweli 3:1, 5-10.

Angalau sasa Yehova alikuwa na mtumishi huko Shilo ambaye alikuwa anamsikiliza. Naye Samweli akawa mtu aliyemsikiliza Yehova nyakati zote. Namna gani wewe? Si lazima tungojee sauti isiyo ya kawaida itokee usiku kuzungumza nasi. Leo, sikuzote sauti ya Mungu huongea nasi kwa njia fulani. Sauti hiyo inapatikana katika Neno lake lililokamilika, Biblia. Kadiri tunavyoendelea kumsikiliza Mungu na kutenda kulingana na yale anayotambua, ndivyo imani yetu inavyoongezeka. Hivyo ndivyo ilivyotokea kwa Samweli.

Usiku huo ulikuwa wa maana sana katika masha ya Samweli, kwa sababu alianza kumjua Yehova katika njia ya kipekee na akawa nabii na mse maji wake. Mwanzoni, mvulana huyo aliogopa kumpa Eli ujumbe wa Yehova, kwa sababu ulikuwa tangazo la mwisho la kwamba unabii uliohusu familia hiyo ungetimizwa. Lakini Samweli alizungumza na Eli kwa ujasiri, naye Eli akakubali kwa unyenyekevu hukumu hiyo ya Mungu. Muda si muda, kila kitu ambacho Yehova alisema kilitimizwa. Waisraeli walipigana na Wafilisti, na Hofni na Finehasi wakauawa siku hiyohiyo. Naye Eli akafa baada ya kujua kuwa Sanduku takatifu la Agano lilikuwa limetekwa.—1 Samweli 3:10-18; 4:1-18.

Lakini sifa nzuri za Samweli akiwa nabii mwaminifu wa Mungu zilizidi kuongezeka. Simulizi hilo linasema, “Yehova akawa pamoja naye,” na kuongezea kuwa Yehova aliendelea kutimiza kila unabii ambao Samweli alitoa.—1 Samweli 3:19.

‘Samweli Alimwita Yehova’

Hata hivyo, je, hilo linamaanisha kwamba Waisraeli walifuata mwongozo wa Samweli na kuwa watu wa kiroho na waaminifu? Hapana. Baada ya muda, waliamua kuwa hawakutaka kuongozwa na nabii tu. Walitaka kuwa kama mataifa mengine na kutawaliwa na mfalme wa kibinadamu.

Ingawa Samweli aliogopa, bado alimweleza Eli kuhusu ujumbe wa hukumu ambao Yehova alitoa





Kwa mwongozo wa Yehova, Samweli alifanya kama wali-vyotaka. Lakini alihitaji kuwaonyesha Waisraeli uzito wa dhambi yao. Hawakuwa wanamkataa mwanadamu tu, bali Yehova mwenyewe! Kwa hiyo akawaita Waisraeli huko Gilgali.

Acheni tuone jinsi alivyozungumza na Waisraeli huko Gilgali wakati huo mgumu. Samweli aliwakumbusha Waisraeli kuhusu maisha yake ya uaminifu. Kisha, tunasoma hivi: “Samweli akamwita Yehova.” Akamwomba alete

Samweli alisali akiwa na imani, naye Yehova akajibu kwa kuleta ngurumo na mvua

ngurumo na mvua.—1 Samweli 12:17, 18.

Kwa nini alete ngurumo na mvua wakati wa kiangazi? Hilo ni jambo lisilowezekana! Kama watu walikuwa na shaka yoyote au walimdhihakiki Samweli, hawakufanya hivyo kwa muda mrefu. Ghafla mawingu meusi yalitanda angani. Upepo ukaanza kuvuma, na kuharibu ngano shambani. Nayo radi ikatoa ngurumo kwa kishindo. Na mvua ikanyesha. Watu walifanya nini? ‘Waliwaogopa sana Yehova na Samweli.’ Mwishowe, wakatabua uzito wa dhambi yao.—1 Samweli 12:18, 19.

Yehova, Mungu wa Samweli ndiye aliyefikia mioyo yao yenye kuasi, bali si Samweli. Samweli aliweka imani yake kwa Mungu tangu alipokuwa kijana hadi alipozeeka. Na Yehova alimbariki. Hata leo, Yehova hajabadilika. Bado huwategemeza wale wanaoiga imani ya Samweli.



JINSI UNAVYOWEZA KUZUIA Hisia Zisizofaa

JE, WEWE unapambana na hisia zisizofaa? Bila shaka, sote tunakabili hisia hizo. Leo kuna matatizo ya kiuchumi, jeuri nyingi, na ukosefu wa haki unaozidi kuumiza watu wengi. Haishangazi kuwa watu wengi sana wamelemewa na hisia za huzuni, hatia, na hali ya kuhisi kuwa hawafai.

Hisia kama hizo zinaweza kuwa hatari sana. Zinaweza kufanya tusijiamini, tupoteze uwezo wa kufikiri vizuri, na hata kutunyang'anya furaha yetu. Biblia inasema hivi: “Je, umejionyesha kuwa umevunjika moyo siku ya taabu? Nguvu zako zitakuwa chache.” (Methali 24:10) Tunahitaji kuwa na nguvu ili tuweze kupambana na ulimwengu huu wenye matatizo. Hivyo ni muhimu sana kudhibiti hisia zisizofaa.*

Biblia inaandaa mwongozo thabiti unaoweza kutusaidia kushinda hisia zisizofaa. Yehova Mungu, ambaye ni Muumba na Mtegemezaji wa uhai wote, hataki tushindwe na hisia zisizofaa wala tukose tumaini. (Zaburi 36:9) Acheni tuchunguze njia tatu ambazo Neno lake linaweza kutusaidia kupambana na hisia hizo.

Tambua Kwamba Mungu Anakujali

Watu fulani hufikiri kuwa Mungu ana shughuli nyingi sana hivi kwamba hawezi kuka- zia fikira hisia za kila mmoja wetu. Je, hivyo ndivyo unavyohisi? Biblia inatuhakikishia kwamba Muumba wetu anajali sana hisia zetu. Mtu- nga-zaburi aliandika hivi: “Yehova yuko kari- bu na wale waliovunjika moyo; naye huwaokoa wale waliopondwa roho.” (Zaburi 34:18) Inafari- riji kama nini kujua kwamba Mwenye Enzi Kuu

* Wale ambao wamekuwa na tatizo la kushuka moyo kwa muda mrefu wanapaswa kumwona daktari.—Mathayo 9:12.

na mweza yote yuko tayari kutusaidia tunapoka- bili hali ngumu!

Mungu anatumia sana. Biblia inasema kwa- mba “Mungu ni upendo.” (1 Yohana 4:8) Ana- wapenda wanadamu na anawajali wanaoteseka. Kwa mfano, Waisraeli walipokuwa utumwa- ni huko Misri miaka 3,500 hivi iliyopita, Mu- ngu alisema: “Pasipo shaka nimeyaona mateso ya watu wangu walio Misri, nami nimesikia ki- lio chao kwa sababu ya wale wanaowalazimisha kufanya kazi; kwa sababu *na- yajua vizuri maumivu waliyo nayo*. Nami ninashuka ili kuwa- komboa.”—Kutoka 3:7, 8.

Mungu anajua hisia zetu vi- zuri sana kwa sababu, “yeye ndiye aliyetufanya, wala si sisi wenyewe.” (Zaburi 100:3) Hi- vyo, tunapohisi kwamba wa- nadamu wenzetu hawatuelewi, tunaweza kuwa na hakika kuwa Mungu anatumia. Neno la Mungu linasema: “Mungu haoni kama mwanadamu anavyoona, kwa maana mwanadamu huona kile kinachoo- nekana kwa macho, lakini Yehova huona ji- nsi moyo ulivyo.” (1 Samweli 16:7) Mungu ana uwezo wa kuona hata hisia zetu za ndani kabisa.

Bila shaka, Yehova anaona makosa na kasoro zetu. Lakini tunaweza kushukuru kuwa Mu- mba wetu mwenye upendo anasamehe. Dau- di, mwandikaji wa Biblia aliyeongozwa na roho ya Mungu, alisema: “Kama vile baba anavyo- waonyesha wanawe rehema, ndivyo ambavyo Yehova amewaonyesha rehema wale wanao- mwogopa. Kwa maana yeye mwenyewe analijua vema umbo letu, akikumbuka kwamba sisi ni

“Nayajua vizuri maumivu waliyo nayo.”

KUTOKA 3:7, 8

mavumbi.” (Zaburi 103:13, 14) Mungu anatuona kwa njia tofauti na jinsi tunavyojiona. Yeye huzingatia sifa zetu nzuri na kupuuza sifa zile mbaya, mradi tu tunatubu dhambi zetu.—Zaburi 139:1-3, 23, 24.

Hivyo, tunapojihisi hatufai, tunahitaji kuazi-mia kupambana na hisia hizo. Lazima tukumbuke jinsi Mungu anavyotuona!—1 Yohana 3:20.

Sitawisha Urafiki wa Karibu na Mungu

Tunafaidika jinsi gani tunapojiona kama Mungu anavyotuona? Itakuwa rahisi kuchukua hatua nyingine inayoweza kutusaidia kushinda hisia zisizofaa, yaani, kusitawisha urafiki wa karibu pamoja na Mungu. Je, hilo linawezekana?

Kama Baba mwenye upendo, Yehova Mungu yuko tayari kutusaidia kusitawisha urafiki wa karibu pamoja naye. Biblia inatuhimiza hivi: “Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia ninyi.” (Yakobo 4:8) Hebu fikiria jambo hili la hakika: Ingawa sisi ni dhaifu na wenye dhambi, bado tunaweza kusitawisha urafiki wa karibu pamoja na Mwenye Enzi Kuu ya ulimwengu wote mzima.

Mungu amejifunua mwenyewe katika Biblia ili tuweze kumjua vizuri. Kwa kuisoma Biblia kwa ukawaida, tunaweza kujifunza sifa za Mungu zenye kuvutia.* Tunapotafakari mambo tunayojifunza kumhusu, tutaende-

lea kuwa na uhusiano wa karibu pamoja naye. Tutaelewa vizuri zaidi kwamba yeye kwa kweli ni Baba mwenye upendo na huruma.

Kutafakari kwa undani yale tunayojifunza katika Biblia kutatusaidia hata zaidi. Tunamkaribia Baba yetu wa mbinguni kwa kuruhu-


* Gazeti la *Mnara wa Mlinzi* la Agosti 1, 2009 (1/8/2009) lina ratiba nzuri inayoweza kukusaidia kusoma Biblia.

su maoni yake yaingie katika akili na mioyo yetu, na kukubali yaturekebishe, yatufariji, na kutuongoza. Tunahitaji kufanya hivyo hasa tunapopambana na mawazo na hisia zinazotusumbua au kutufadhaisa. Mtunga zaburi alisema hivi: “Mahangaiko ya moyo wangu yanapozi-di, wewe wanifariji na kunifurahisha.” (Zaburi 94:19, *BHN*) Neno la Mungu linaweza kutufariji sana. Ikiwa tutakubali Neno la Mungu kwa unyenyekevu, huenda hisia zetu zisizofaa zikabadilika na tukapata faraja na amani ambayo Mungu pekee ndiye aliye na uwezo wa kuitoa. Hivyo, Yehova anatufariji kama mzazi mwenye upendo anavyomtuliza mtoto ambaye amemia au kukasirika.

Jambo lingine linaloweza kutusaidia kuwa rafiki za Mungu ni kuongea naye kwa ukawaida. Biblia inatuhakikishia ya kwamba “hata tukio-mba nini kulingana na mapenzi yake, [Mungu] hutusikia.” (1 Yohana 5:14) Hata tuwe na mahangaiko ya aina gani, tunaweza kumwomba Mungu atusaidie. Tukimweleza yaliyo moyoni mwetu, tunapata amani ya akili. Mtume Paulo aliandika hivi: “Katika kila jambo kwa sala na

“Mahangaiko ya moyo wangu yanapozidi, wewe wanifariji na kunifurahisha.”

ZABURI 94:19,
BIBLIA HABARI NJEMA



dua pamoja na kutoa shukrani maombi yenu na yajulishwe Mungu; na *amani ya Mungu yenye ubora unaozidi fikira zote itailinda mioyo yenu na nguvu zenu za akili* kwa njia ya Kristo Yesu.” —Wafilipi 4:6, 7.

Unapoendelea kufuata ratiba ya kusoma Biblia, kutafakari, na kusali kibinafsi, bila shaka, utajenga uhusiano wa karibu pamoja na Baba yako wa mbinguni. Uhusiano huo wa karibu ni silaha inayoweza kutusaidia kupambana na hisia zisizofaa. Ni jambo gani lingine linaloweza kukusaidia?

Kazia Fikira Tumaini Hakika la Wakati Ujao

Hata tukabili hali ngumu kiasi gani, bado tunaweza kukazia fikira mambo mazuri. Jinsi gani? Mungu ametupa tumaini hakika la wakati ujao. Mtume Petro alisema hivi kuhusu tumaini hilo zuri: “Kulingana na ahadi [ya Mungu] tunaongojea mbingu mpya na dunia mpya, na humo uadilifu utakaa.” (2 Petro 3:13) Hilo linamaanisha nini?

Maneno “mbingu mpya” yanamaanisha serikali, yaani, Ufalme wa mbinguni wa Mungu

unaoongozwa na Yesu Kristo. “Dunia mpya” inamaanisha jamii mpya ya wanadamu iliyokubaliwa na Mungu ambayo itaishi hapa duniani. Chini ya utawala wa “mbingu mpya,” jamii mpya ya kidunia haitapatawa na mambo yanayosababisha hisia zisizofaa.

Kuhusu wanadamu waminifu watakaishi wakati huo, Biblia inatahakikishia kwamba Mungu “atafuta kila chozi kutoka katika macho yao, na kifo hakitakuwapo tena, wala maombolezo wala kilio wala maumivu hayatakuwapo tena.”—Ufunuo 21:4.

Kwa kweli, hayo ni mambo yenye kuchangamsha na kutia moyo sana. Hiyo ndiyo sababu Biblia inataja kwamba ahadi za wakati ujao ambazo Mungu amewapa Wakristo wa kweli, ni “tumaini la furaha.” (Tito 2:13) Tunapokazia fikira ahadi za Mungu za wakati ujao kwa wanadamu—na sababu zinazofanya

“Amani ya Mungu yenye ubora unaozidi fikira zote itailinda mioyo yenu na nguvu zenu za akili.”

WAFILIPU 4:7

Maandiko Yenye Kufaraji Kumhusu Yehova Mungu

“Yehova, Mungu mwenye rehma na neema, si mwepesi wa hasira naye ni mwingi wa fadhili zenye upendo na kweli.” —KUTOKA 34:6.

“Macho yake yanaenda huku na huku duniani kote ili aonyeshe nguvu zake kwa ajili ya wale ambao moyo wao ni mkamilifu kumwelekea yeye.” —2 MAMBO YA NYAKATI 16:9.

“Yehova yuko karibu na wale waliovunjika moyo; naye hu-

waokoa wale waliopondwa roho.”—ZABURI 34:18.

“Ee Yehova, ni mwema na uko tayari kusamehe.”—ZABURI 86:5.

“Yehova ni mwema kwa wote, na rehema zake ziko juu ya kazi zake zote.”—ZABURI 145:9.

“Mimi, Yehova Mungu wako, ninaushika mkono wako wa kuume, Mwenye kukuambia, ‘Usiogope. Mimi mwenyewe nitakusaidia.’”—ISAYA 41:13.

“Abarikiwe . . . Baba ya rehma nyororo na Mungu wa faraja yote.”—2 WAKORINTHO 1:3.

“Tutaihakikishia mioyo yetu mbele zake kwa habari ya lolote ambalo huenda mioyo yetu ikatuhukumu kuwa na hatia, kwa sababu Mungu ni mkuu kuliko mioyo yetu naye anajua mambo yote.”—1 YOHANA 3:19, 20.

tuamini kuwa ahadi hizo zinategemeka na ni za kweli—tunayasukuma mbali mawazo yasiyofaa.—Wafilipi 4:8.

Biblia hufananisha tumaini letu la wokuwu na kofia ya chuma. (1 Wathesalonike 5:8) Katika nyakati za kale, askari jeshi hangeenda vitani bila kofia ya chuma. Alijua kwamba kofia hiyo ingemzuia asiumie anapogongwa kichwani na kitu chochote kile. Kama vile kofia ya chuma inavyolinda kichwa, ndivyo tumaini

linavyolinda akili. Tunapoendelea kufikiria mambo yanayotusaidia kuwa na tumaini, tunalindwa ili tusiwe na woga na mawazo yasiyofaa.

Kwa hiyo, inawezekana kushinda hisia zisizofaa. Bila shaka, hata wewe unaweza kufanya hivyo! Tafakari jinsi Mungu anavyokuona, mkaribie, na ukazie fikira tumaini lako la wakati ujao. Hivyo, unaweza kuwa na hakika kwamba utaiishi wakati ambapo watu hawatapambana kamwe na hisia zisizofaa!—Zaburi 37:29.



Wamefaulu Kupambana na Hisia Zisizofaa

“Baba yangu ni mlevi wa kupindukia, na amenifanya niteseke sana. Kwa muda mrefu nimekuwa nikihihi kuwa safai. Lakini nilipokubali kujifunza Biblia pamoja na Mashahidi wa Yehova, nilijifunza kuhusu tumaini la uzima wa milele duniani. Kwa sababu ya tumaini hilo, nilijawa na furaha akilini na moyoni mwangu. Nilianza kusoma Biblia kwa ukawaida. Mimi huwa na Biblia kila mara. Ninapoanza kuwa na hisia zisizofaa, mimi huifungua na kusoma maandiko yenye kutia moyo. Kusoma kuhusu sifa zenye kuvutia za Mungu hunihakikishia jinsi nilivyo na thamani machoni pake.”—*Kátia, mwanamke mwenye umri wa miaka 33.**

“Nilikuwa mlevi kupindukia, mraibu wa bangi, kokeini, kokeini kali, na nilinusa gundi. Baada ya kupoteza kila kitu nilichokuwa nacho, nilianza kuomba-omba. Lakini baada ya kukubali kujifunza Biblia na Mashahidi wa Yehova, nilibadili maisha yangu kabisa. Nikawa na uhusiano wa karibu pamoja na Mungu. Ingawa bado mimi ninapambana na hali ya kujihisi nina hatia au safai, nimejifunza kutegemea rehema na fadhili zenye upendo za Mungu. Nina hakika kuwa Mungu ataendelea kunipa nguvu za kushinda hisia zisizofaa. Kujua kweli za Biblia ndilo jambo zuri zaidi kuwahi kutukia maishani mwangu.”—*Renato, mwanamume mwenye umri wa miaka 37.*

“Tangu nilipokuwa kijana mdogo, nilikuwa nikijilinganisha na ndugu yangu mkubwa. Nilijihisi duni mbele zake. Bado mimi hujihisi siko salama na sijiamini. Lakini nimeazimia kushinda pambano hilo. Nimesali kwa Yehova bila kuacha, naye amenisaidia kushinda hali ya kujihisi safai. Inatia moyo kama nini kujua kuwa Mungu ananipenda na ananijali kikweli!”—*Roberta, mwanamke mwenye umri wa miaka 45.*



MKARIBIE MUNGU

“Msikiaji wa Sala”

1 MAMBO YA NYAKATI 4:9, 10

JE, KWELI Yehova Mungu hujibu sala za unyofu za waabudu waliojitoa kwake? Simulizi la Biblia kuhusu mtu asiyejulikana sana aitwaye Yabesi, linaonyesha kuwa Yehova kwa kweli ni “msikiaji wa sala.” (Zaburi 65:2) Simulizi hilo fupi linapatikana mahali ambapo mtu hangetazamia kulipata—katika orodha za kiukoo zinazopatikana mwanzoni mwa kitabu cha Kwanza cha Mambo ya Nyakati. Acheni tuchunguze 1 Mambo ya Nyakati 4:9, 10.

Mambo yote tunayojua kumhusu Yabesi yapatikana katika mistari hiyo miwili. Kulingana na mstari wa 9, mama yake ‘alimwita jina Yabesi, akisema: “Nimemzaa kwa maumivu.”* Kwa nini alichagua jina hilo? Je, alimzaa mwana huyo kwa maumivu makali zaidi kuliko ilivyo kawaida? Je, labda alikuwa mjane aliyehuzunika kwamba mumewe hakuwa hai kumwona mtoto wao mchanga? Biblia haijibu maswali hayo. Lakini siku moja mama huyo angekuwa na sababu ya kujivunia mtoto wake. Huenda ndugu za Yabesi walikuwa watu wenye kuheshimika, lakini “Yabesi a[liku]ja kuheshimika kuliko ndugu zake.”

Yabesi alipenda kusali. Alianza sala yake kwa kuomba baraka za Mungu. Kisha, akaomba mambo matatu yanayoonyesha alikuwa na imani thabiti.

Kwanza, Yabesi alimwomba Mungu, akisema: “Upanue eneo langu.” (Mstari wa 10) Mtu huyu mwenye kuheshimika hakuwa mnyakuzi wa ardhi, aliyetamani vitu vya watu wengine. Huenda ombi lake lilihusu watu hasa, bali si ardhi. Huenda alikuwa akiomba eneo lake

* Jina Yabesi linatokana na neno linaloweza kumaanisha “maumivu.”

lipanuliwe kwa amani ili apate nafasi ya kutosha kwa ajili ya waabudu wa Mungu wa kweli.*

Pili, Yabesi aliomba ‘mkono’ wa Mungu uwe pamoja naye. Mkono huo wa mfano unamaanisha nguvu za Mungu, ambazo anatumia kuwasaidia waabudu wake. (1 Mambo ya Nyakati 29:12) Ili ajibiwe maombi ya moyo wake, Yabesi alimtegemea Mungu ambaye mkono wake si mfupi kuwaelekea wale wanaomwamini.—Isaya 59:1.

Tatu, Yabesi aliomba hivi: “Uniokoe kutoka katika msiba, ili huo usipate kunidhuru.” Huenda maneno “usipate kunidhuru” yanadokeza kwamba Yabesi aliomba, si aepuke msiba, bali ali ndwe ili asihuzunishwe wala asishindwe na matokeo ya uovu.

Sala ya Yabesi ilionyesha kuwa alihangaikia ibada ya kweli na alimwamini na kumtumaini Msikiaji wa sala. Yehova alifanya nini? Simulizi hili fupi linalamaliza kwa maneno: “Basi Mungu akatimiza yale ambayo yeye alikuwa ameomba.”

Msikiaji wa sala hajabadilika. Yeye hufurahia sala za waabudu wake. Wale wanaomwamini na kumtumaini wanaweza kuwa na uhakika huu: “Hata tukiomba nini kulingana na mapenzi yake, yeye hutusikia.”—1 Yohana 5:14.

* Katika Targumi, au tafsiri za Wayahudi za Maandiko Matakatifu yaliyofafanuliwa, maneno ya Yabesi yametafsiriwa hivi: “Nibariki kwa kunipa watoto, na upanue mipaka yangu kwa kunipa wanafunzi.”





WAFUNDISHE WATOTO WAKO

Ufalme Ambao Utabadili Dunia Nzima

JE, UNAJUA ni Ufalme gani tunaozungumzia?—* Ni ule ambao Yesu alitufundisha tuombe uje. Alitufundisha tumwombe Mungu hivi: “Ufalme wako na uje.” (Mathayo 6:9, 10) Kwa karibu miaka 2,000, wafuasi wa Yesu wamekuwa wakimwomba Mungu kwamba Ufalme Wake uje. Je, umewahi kuomba ufalme huo uje?—

Ili kuelewa ufalme ni nini, unahitaji kujua mfalme ni nani. Mfalme ni mtu anayetawala. Na nchi anayotawala inaitwa miliki yake. Miliki ya Ufalme wa Mungu inatia ndani *dunia nzima*. Ufalme wa Mungu utakapokuja, kila mtu duniani atafurahia baraka ambazo utawala huo utawaletea wana-damu.

Ufalme wa Mungu ni serikali ya mbinguni. Katika andiko la Isaya 9:6, Biblia inamtaja Mtawala wa serikali hiyo. Ona vile linavyosema kumhusu: “Kuna mtoto ambaye amezaliwa kwetu, . . . na *utawala wa ukuu* utakuwa juu ya bega lake. Naye ataitwa jina . . . Mkuu wa Amani [au mwana-mfalme wa amani].”

Je, unajua mkuu, au mwana-mfalme, ni nani?— Ndiyo, ni mtoto wa kiume wa mfalme. Ni nani Mfalme mkuu zaidi mbinguni?— Jibu lako ni sahihi ukisema ni Yehova. Biblia inasema yeye ndiye ‘Aliye Juu Zaidi, juu ya dunia yote.’ (Zaburi 83:18) Katika Biblia, mara nyingi Yesu anaitwa “Mwana wa Mungu.” Sababu moja ya kuitwa hivyo

* Kama unasoma sehemu hii pamoja na mtoto, unapona kistari kama hiki (—), tua na umtie moyo mtoto atoe maoni yake.



ni kwamba Yehova ndiye aliyempa uhai. Yehova ndiye hasa Baba ya Yesu.—Luka 1:34, 35; Yohana 1:34, 49; 3:17; 11:27; 20:31; Matendo 9:20.

Ufalme wa Mungu, ambao Yesu alitufundisha tuombe uje, ni serikali ya kipekee sana. Ni “utawala wa ukuu” kwa sababu Yehova anamfanya Mwana wake Yesu kuwa Mtawala, au Mfalme, wa Ufalme huo. Lakini je, unajua kwamba watu wengine watachaguliwa kutawala wakiwa wafalme pamoja na Yesu katika Ufalme wa Baba yake?— Hebu tuzungumze kuhusu watu hao.

Muda mfupi kabla ya kufa, Yesu aliwambia mitume wake waaminifu kwamba alikuwa anaenda katika “nyumba” ya Baba yake huko mbinguni. “Ninaenda kuwatayarishia ninyi mahali,” akasema, “ili mahali nilipo mimi, ninyi pia muwe hapo.” (Yohana 14:1-3) Je, unajua mitume na watu we-



ngine ambao wamechaguliwa watafanya nini mbinguni pamoja na Yesu?— “Watatawala wakiwa wafalme pamoja naye.” Biblia hata inatuambia ni watu wangapi watakaotawala pamoja na Yesu. Watakuwa 144,000.—Ufunuo 14:1, 3; 20:6.

Unafikiri hali zitakuwa namna gani duniani wakati Mkuu wa Amani na wale 144,000 aliowachagua watakapotawala?— Hali zitakuwa nzuri wee! Hakuwakuwa na vita. Kutakuwa na amani kati ya wanyama wenyewe na pia kati ya wanyama na wanadamu. Hakuna mtu atakayekuwa mgonjwa wala kufa. Macho ya wasioweza kuona yataona, masikio ya wasioweza kusikia yatasikia, mtu aliye kilema ataruka kama paa. Dunia itatokeza chakula

kizuri kwa ajili ya kila mtu. Na watu wote watapendana kama vile Yesu alivyowafundisha wanafunzi wake wafanye. (Yohana 13:34, 35) Hebu tusome mistari iliyoorodheshwa hapa kutoka katika kitabu cha Isaya na tuone mambo mazuri ambayo yatatokea.—Isaya 2:4; 11:6-11; 25:8; 33:24; 35:5, 6; 65:21-24.

Tangu Yesu alipowafundisha watu wao mbe “ufalme wako na uje,” mamilioni ya watu wamejifunza kuhusu Ufalme huo. Ujuzi huo umebadili maisha yao. Hivi karibuni wakati Ufalme huo utakapokuja na kuondoa serikali zote duniani, kila mtu anayemtumikia Yehova Mungu na Mtawala wake aliymchagua, Yesu Kristo, atakuwa na amani, afya nzuri, na furaha.—Yohana 17:3.

MASWALI:

- Kwa nini Ufalme wa Mungu pia unaitwa “utawala wa ukuu”?
- Ni nani watakaotawala pamoja na Yesu katika Ufalme wa Baba yake?
- Hali zitakuwa namna gani duniani chini ya utawala wa Yesu?



MASHAHIDI WA YEHOVA hufurahia kuzungumza kuhusu Biblia pamoja na jirani zao. Je, una swali lolote la Biblia ambalo limekuwa likikutatiza? Je, kuna jambo lolote ambalo Mashahidi wa Yehova wanaamini au kufanya ambalo ungependa kulifahamu zaidi? Ikiwa ndivyo, basi unapokutana tena na Shahidi wa Yehova usikose kumwuliza. Yeye atafurahi kuzungumzia jambo hilo pamoja nawe.

Mazungumzo Pamoja na Jirani

Roho Takatifu Ni Nini?

Mazungumzo yaliyo hapa chini yanaonyesha jinsi Shahidi wa Yehova anavyoweza kuzungumza na jirani yake. Hebu tuwazie kwamba Shahidi anayeitwa Joshua amemtembelea mwanamume anayeitwa Daniel nyumbani kwake.

Unamaanisha Nini Unaposema “Roho Mtakatifu”?

Daniel: Nimesikia kwamba nyinyi Mashahidi wa Yehova si Wakristo kwa sababu hamwamini roho mtakatifu.

Joshua: Kwanza, ningependa kukuhakikishia kwamba sisi ni Wakristo. Nimekuja kwako asubuhi ya leo kwa sababu ninamwamini Yesu Kristo. Yeye ndiye anayewaamuru wafuasi wake wahubiri. Lakini hebu nikuulize, unamaanisha nini unaposema “roho mtakatifu”?

Daniel: Ninamaanisha yule mtu wa tatu katika Utatu, msaidizi ambaye Yesu aliahidi atatutumia. Msaidizi huyo ni muhimu sana kwangu. Ninataka kuhisi kwamba roho mtakatifu anatenda kazi katika maisha yangu.

Joshua: Hayo ndiyo maoni ya watu wengi kuhusu roho takatifu. Wakati fulani uliopita nilipata nafasi ya kuchunguza yale ambayo Biblia inafundisha kuhusu jambo hilo. Ikiwa

una dakika chache, nitafurahi kukuonyesha yale niliyojifunza.

Daniel: Ndio, nina dakika kadhaa.

Joshua: Jina langu ni Joshua. Na wewe unaitwa nani?

Daniel: Naitwa Daniel na nimefurahi kukujua.

Joshua: Nimefurahi kukujua pia, Daniel. Ili nisitumie wakati wako mwingi, nitazungumzia jambo moja tu kuhusiana na habari hii. Ulitaja kwamba roho takatifu ndiye msaidizi ambaye Yesu alituahidi. Ninakubaliana nawe. Lakini je, unamaanisha kwamba roho takatifu ni mtu na yeye ni sawa na Mungu?

Daniel: Naam, hivyo ndivyo nilivyofundishwa.

Je, Roho Takatifu Ni Mtu?

Joshua: Acha tuchunguze simulizi fulani katika Biblia ambalo litatusaidia kuona ikiwa roho takatifu ni mtu au si mtu. Huenda unafahamu mistari hii. Tunasoma hivi katika Mateo 2:1-4: “Basi siku ya sherehe ya Pentekoste ilipokuwa ikiendelea walikuwa wote pamoja mahali pale pale, na ghafula kukatokea kutoka mbinguni kelele kama ile ya upepo wenye

nguvu unaovuma, nao ukaijaza nyumba yote ambamo walikuwa wameketi. Nao wakaona ndimi kama za moto, nazo zikagawanyika huku na huku, na mmoja ukaketi juu ya kila mmoja wao, nao wote wakajazwa roho takatifu wakaanza kusema katika lugha tofauti, kama vile roho ilivyokuwa ikiwawezesha kusema.”

Daniel: Ninalifahamu vizuri simulizi hilo.

Joshua: Hivyo, unaonaje Daniel, mtu ana-weza kujazwa na mtu mwingine?

Daniel: Haiwezekani.

Joshua: Hebu tusome mstari mwingine kati-ka sura hiyohiyo—mstari wa 17. Sehemu ya kwanza ya mstari huo inasema: “‘Katika siku za mwisho,’ Mungu asema, ‘Nitaimimina sehemu ya roho yangu juu ya kila namna ya mwili.’” Daniel, hebu nikuulize, Mungu anaweza kumimina sehemu ya Mungu aliye sawa naye?

Daniel: Hapana.

Joshua: Yohana Mbatizaji alitumia njia to-fauti kufafanua kuhusu kujazwa na roho takatifu. Ufafanuzi huo unapatikana katika Mathayo 3:11. Tafadhali ungependa kusoma mstari huo?

Daniel: “Mimi ninawabatiza ninyi kwa maji kwa sababu ya toba yenu; lakini yule anayekuja nyuma yangu ana nguvu kuliko mimi, ambaye viatu vyake mimi sistahili kuvivua. Huyu atawabatiza ninyi kwa roho takatifu na kwa moto.”

Joshua: Asante. Umeona Yohana Mbatizaji alisema roho takatifu ingetumiwa kufanya nini?

Daniel: Alitaja kuhusu kubatizwa kwa roho takatifu.

Joshua: Ni kweli. Ona pia kwamba alitaja kuhusu kubatizwa kwa moto. Ni wazi kwamba moto si mtu. Je, unafikiri mstari huo unaonyesha kwamba roho takatifu ni mtu?

Daniel: Hapana.

Joshua: Kwa hiyo, maandiko ambayo tume-chunguza yanaonyesha kwamba roho takatifu si mtu.

Daniel: Hilo ni kweli.

Ni Katika Njia Gani Roho Takatifu Ni “Msaidizi”?

Joshua: Mwanzoni ulitaja kuhusu “msaidizi.” Yesu alitaja kwamba roho takatifu ni “msaidizi” kwenye Yohana 14:26. Hebu tusome andiko hilo pamoja: “Msaidizi, roho takatifu, ambayo Baba atatuma katika jina langu, hiyo itawafundisha ninyi mambo yote na kuwakumbusha mambo yote niliyowambia.” Watu fulani wanafikiri kuwa andiko hilo linathibitisha wazo la kwamba roho takatifu ni mtu, ambaye atawasaidia na kuwafundisha.

Daniel: Ndiyo, hivyo ndivyo ninavyoamini.

Joshua: Lakini je, inawezekana kwamba Yesu alikuwa akizungumza kwa njia ya mfano? Ona jambo ambalo Yesu alisema kuhusu hekima, katika Luka 7:35: “Hata hivyo, hekima huonyeshwa kuwa yenye uadilifu kwa watoto wake wote.” Je, ungesema kwamba hekima ni mtu, aliye na watoto?

Daniel: Hapana. Hapo alikuwa akizungumza kwa njia ya mfano.

Joshua: Ni kweli. Yesu alikuwa akimaanisha kwamba hekima huonekana kupitia matunda yake. Mara nyingi Biblia hutumia usemi wa mfano unaoitwa tashihisi—yaani, kuzungumzia kitu kisicho na uhai kana kwamba kina uhai. Mara nyingi sisi hutumia semi za mfano katika mazungumzo yetu. Kwa mfano, asubuhi kama ya leo ambapo jua limeangaza, ni kawaida mtu kusema, “Fungua pazia ili mwangaza wa jua uingie,” sivyo?

Daniel: Bila shaka.

Joshua: Je, ungekuwa unamaanisha kwamba mwangaza wa jua ni mtu ambaye ana-weza kuingia ndani ya nyumba yako kama mgeni?

Daniel: Hapana. Huo ni usemi wa mfano.

Joshua: Kwa hiyo, Yesu aliposema kwamba roho takatifu ni msaidizi, au mwalimu, je, inawezekana alikuwa akitumia usemi wa mfano?

Daniel: Nafikiri hivyo. Hilo linapatana na maandiko uliyosoma kwamba roho takatifu

ilimwagwa na kwamba watu walibatizwa kwa roho hiyo. Lakini ikiwa roho takatifu si mtu, ni nini?

Roho Takatifu Ni Nini?

Joshua: Kwenye Matendo 1:8, Yesu anatumia roho takatifu ni nini. Ungependa kusoma mstari huo?

Daniel: “Mtapokea nguvu wakati roho takatifu itakapofika juu yenu, nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu na pia katika Yudea yote na Samaria na mpaka sehemu ya mbali zaidi ya dunia.”

Joshua: Ona kwamba Yesu anahusianisha roho takatifu na nguvu. Na kulingana na mstari tuliyotangulia kusoma, unafikiri nguvu hiyo inatoka wapi?

Daniel: Inatoka kwa Mungu, Baba.

Joshua: Ni kweli. Roho takatifu ndiyo nguvu ileile ambayo Mungu alitumia kuumba ulimwengu. Mstari wa pili wa Biblia unazungumza kuhusu nguvu hiyo. Andiko la Mwanzo 1:2 linasema: “Nguvu za utendaji za Mungu zilikuwa zikienda huku na huku juu ya uso wa maji.” Neno la Kiebrania linalotafsiriwa hapa kuwa “nguvu za utendaji” linatafsiriwa pia kuwa “roho.” Roho hiyo ni nguvu zisizoonekana za utendaji ambazo Mungu hutumia kutimiza kusudi lake na kufunua mapenzi yake. Acha nikuonyeshe andiko lingine moja tu—Luka 11:13. Tafadhali, ungependa kusoma mstari huu?

Daniel: “Ikiwa ninyi, mhapokwa waovu, mnajua jinsi ya kuwapa watoto wenu zawadi zilizo njema, je, Baba aliye mbinguni hatawapa hata zaidi roho takatifu wale wanaomwomba!”

Joshua: Ikiwa Baba aliye mbinguni ndiye mwenye mamlaka juu ya roho takatifu, na anawapa wale wanaomwomba, je, roho takatifu inaweza kuwa sawa na Baba?

Daniel: Hapana. Nimeelewa unachosema.

Joshua: Sitaki kutumia wakati wako mwingi, Daniel. Ulisema kwamba una dakika cha-

che tu. Lakini acha nikuulize swali la mwisho. Kutokana na maandiko ambayo tumesoma, ungesema roho takatifu ni nini?

Daniel: Ni nguvu za utendaji za Mungu.

Joshua: Ni kweli. Na kulingana na Yohana 14:26, Yesu alipozungumza kuhusu roho takatifu kuwa msaidizi, au mwalimu, alikuwa aki-tumia usemi wa mfano unaoitwa tashihisi.

Daniel: Sikujua hilo.

Joshua: Kuna jambo lenye kufariji sana ambalo tunajifunza kutokana na maneno ya Yesu.

Daniel: Jambo gani hilo?

Joshua: Tunaweza kumwomba Mungu roho yake takatifu ili itusaidie tunapopatwa na hali ngumu. Tunaweza pia kuomba roho yake itusaidie tujifunze ukweli kumhusu.

Daniel: Hilo ni jambo zuri. Nitalifikiria.

Joshua: Kabla sijaondoka, ningependa pia ufikirie jambo hili lingine. Kwa kuwa roho takatifu ni nguvu za utendaji za Mungu, basi tunakubaliana kwamba Mungu anaweza kuitumia kutimiza jambo lolote analotaka.

Daniel: Bila shaka.

Joshua: Hivyo basi, kwa nini hajatumia nguvu hizo zisizo na mipaka kumaliza matatizo na uovu wote tunaona leo ulimwenguni? Umewahi kujiuliza swali hilo?*

Daniel: Nimewahi kujiuliza.

Joshua: Je, itakuwa sawa nikirudi juma lijalo wakati kama huu tuzungumzie jambo hilo?

Daniel: Nitafurahi sana. Tuonane wakati huo.

* Kwa habari zaidi, ona sura ya 11 ya kitabu *Biblia Inafundisha Nini Hasa?* kilichochapishwa na Mashahidi wa Yehova.



UWEZO WA KUSEMA KWA LUGHA JE, UNATOKA KWA MUNGU?


"SIELEWI," anasema Devon. "Kila juma, watu wengi katika kanisa langu huonekana kupokea roho takatifu na kusema kwa lugha mbalimbali kimuujiza. Baadhi yao wanaishi maisha mapotovu. Mimi hujitahidi kuishi kupatana na kanuni za Biblia. Lakini hata nisali kwa bidii kadiri gani, mimi sipati zawadi hiyo ya roho. Kwa nini iwe hivyo?"

Gabriel naye ni mshiriki wa kanisa ambalo waumini wake huonekana kupokea roho takatifu na kusema kwa lugha mbalimbali. Yeye anasema, "Jambo linalonisumbua ni moja. Wakati ninaposali, watu wengine hunikatiza kwa sala wanazotoa kwa sauti kubwa wakitumia maneno ambayo siyaelewi wala wao wenyewe hawayaelewi. Hakuna mtu ambaye hufaidika na sala hizo. Lakini ikiwa zawadi inatokana na roho ya Mungu, si inapaswa kuwa na manufaa?"

Mambo ambayo Devon na Gabriel wamejionea yanatokeza swali lenye kuamsha fikira, Je, ni kweli kwamba uwezo wa kusema kwa lugha, kama ilivyo katika makanisa fulani leo, unatoka kwa Mungu? Ili kujibu swali hilo, inafaa kuchunguza jinsi zawadi ya kimuujiza ya kuzungumza kwa lugha ilivyotumiwa kati ya Wakristo wa karne ya kwanza.

'Walianza Kusema kwa Lugha Mbalimbali'

Katika Biblia, tunasoma kuhusu wanaume na wanawake fulani ambao walipewa uwezo wa kuzungumza kwa lugha ambazo hawakuwa wamewahi kujifunza. Hilo lilitukia kwa mara ya kwanza siku ya Pentekoste 33 W.K., majuma kadhaa baada ya kifo cha Yesu Kristo. Wanafunzi 120 hivi walio kuwa Yerusalemu siku hiyo 'walijazwa roho takatifu wakaanza kusema katika lugha tofauti.' Watu kutoka nchi za kigeni 'walishikwa na bumbuzi, kwa sababu kila mmoja aliwasikia wakisema katika lugha yake mwenyewe.'—Matendo 1:15; 2:1-6.



Biblia pia inataja wafuasi wengine wa Yesu wa karne ya kwanza ambao walikuwa na uwezo huo wa kipekee. Kwa mfano, kwa nguvu za roho takatifu, mtume Paulo aliweza kuzungumza kwa lugha mbalimbali kimuujiza. (Matendo 19:6; 1 Wakorintho 12:10, 28; 14:18) Lakini zawadi kama hiyo ya roho takatifu ya Mungu inapaswa kutolewa kwa kusudi zuri. Kwa hiyo, ni kwa kusudi gani watu katika nyakati za Biblia walipewa uwezo wa kusema kwa lugha mbalimbali?

Ishara ya Kuungwa Mkono na Mungu

Alipowaandikia Wakristo katika jiji la Korintho, ambao baadhi yao wangeweza kuzungumza kwa lugha mbalimbali, Paulo alieleza kwamba "lugha ni kwa ajili ya ishara . . . kwa wasio waumini." (1 Wakorintho 14:22) Kwa hiyo, uwezo

wa kusema kwa lugha, kutia ndani uwezo mbalimbali wa kufanya miujiza, ulikuwa ishara kwa watazamaji kwamba Mungu alilikubali na kuliunga mkono kutaniko jipya la Kikristo lililokuwa limefanyizwa. Zawadi za kimuujiza zilikuwa kama ishara za barabarani ambazo ziliwaelekeza watu waliokuwa wakitafuta kweli wafike mahali walipopaswa kwenda, ili kuwapata watu waliochaguliwa na Mungu.

Ni muhimu kutambua kwamba Biblia haiseimi kuwa Yesu wala nabii yeyote wa kabla ya Ukristo alikuwa na uwezo wa kimuujiza wa kusema kwa lugha ambazo hawakuzijua. Basi, ni wazi kwamba kuna sababu nyingine iliyofanya wanafunzi wa Yesu wapewe zawadi ya kusema kwa lugha mbalimbali.

Zawadi ya Kusema kwa Lugha Yatumiwa Kueneza Habari Njema

Mapema katika huduma yake, Yesu aliwaagiza wanafunzi wake wahubiri habari njema ya Ufalme wa Mungu kwa Wayahudi tu. (Mathayo 10:6; 15:24) Kwa sababu hiyo, wanafunzi walihubiri hasa katika maeneo yaliyokuwa na Wayahudi wengi. Lakini muda si muda, mambo yangebadilika.

Muda mfupi baada ya kifo chake mwaka wa 33 W.K., Yesu aliyefufuliwa aliwaamuru wafuasi wake ‘wakafanye wanafunzi kutoka kwa watu wa mataifa yote.’ Pia, aliwaambia wafuasi wake kwamba wangukuwa mashahidi wake “mpaka sehemu ya mbali zaidi ya dunia.” (Mathayo 28:19; Matendo 1:8) Ili kueneza habari njema kwa kiwango hicho, wanafunzi wangehitaji kutumia lugha nyingine nyingi kando na Kiebrania.

Hata hivyo, wengi kati ya wanafunzi hao wa mapema walikuwa “watu wasio na elimu na wa kawaida tu.” (Matendo 4:13) Hivyo basi, wangezaje kuhubiri katika nchi za mbali ambako watu walizungumza lugha ambazo hawajawahi kuzisikia wala kuzizungumza? Roho takatifu iliwapa baadhi ya wahubiri hao wenye bidii uwezo wa kimuujiza wa kuhubiri kwa ufasaha katika lugha ambazo hawakuzijua.

Kwa hiyo, zawadi ya kusema kwa lugha ilitolewa kwa malengo mawili muhimu. Kwanza, ili-

kuwa ishara kwamba Mungu aliliunga mkono kutaniko la Kikristo. Pili, ilisaidia sana Wakristo wa karne ya kwanza kutimiza utume wao wa kuwahubiria watu wa lugha mbalimbali. Je, wale wanaosema kwa lugha katika makanisa mbalimbali leo wanatimiza malengo hayo?

Kusema kwa Lugha Leo, Je, Ni Ishara ya Kuungwa Mkono na Mungu?

Ungeweka ishara wapi ili kuwasaidia watu wengi iwezekanavyo katika eneo lako? Ndani ya jengo dogo? Hapana! Simulizi kuhusu siku ya Pentekoste linasema kuwa “umati” wa wapitanjia waliona ishara wakati wanafunzi walipozungumza kwa lugha mbalimbali kimuujiza. Kwa sababu hiyo, “nafsi karibu elfu tatu zikaongezwa” katika kutaniko la Kikristo siku hiyo! (Matendo 2:5, 6, 41) Ikiwa leo watu wanaodai kusema kwa lugha wanafanya hivyo tu ndani ya kanisa, jambo hilo linaweza jinsi gani kuwa ishara inayoonekana waziwazi na umati wa wasioamini?

Neno la Mungu linataja uasherati na “mate-ndo [mengine] ya mwili” kuwa yanapingana na utendaji wa roho takatifu, na kuongeza kwamba “wale walio na mazoea ya kufanya mambo ya namna hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu.” (Wagalatia 5:17-21) Iwapo unawaona watu wenye mwenendo mpotovu wakisema kwa lugha, huenda kwa kufaa ukauliza, ‘Je, hilo si jambo lisilowezezana—hata lenye kupotosha—kwa Mungu kuwapa roho takatifu watu walio na mazoea ya kufanya mambo ambayo yanashutumiwa na Neno lake?’ Hilo ni kama kuweka ishara ya barabarani inayopotosha watu.

Je, Kusema kwa Lugha Leo Kunatumia Kueneza Habari Njema?

Namna gani kuhusu lile kusudi lingine la zawadi ya kusema kwa lugha katika karne ya kwanza? Je, kusema kwa lugha katika makanisa leo kunachangia kuenezwa kwa habari njema kwa watu wa lugha mbalimbali? Kumbuka kwamba watazamaji waliokuwa Yerusalemu siku ya Pentekoste 33W.K., walitoka katika nchi nyingi, na walielewa vizuri lugha zilizozungumzwa kimuu-

jiza na wanafunzi. Tofauti na hilo wale wanaosema kwa lugha leo, kwa kawaida husema mambo yasiyoweza kueleweka na yeyote.

Bila shaka, wale wanaosema kwa lugha leo wanafanya hivyo kwa njia tofauti kabisa na jinsi wafuasi wa mapema wa Yesu waliopewa zawadi ya roho takatifu walivyofanya. Hata hakuna uthibitisho wenye kutegemeka kwamba kuna yeyote aliyepokea nguvu hizo za kimuujiza baada ya mitume kufa. Jambo hilo haliwashangazi wasomaji wa Biblia. Kuhusu zawadi za kimuujiza, kutia ndani kusema kwa lugha, mtume Paulo aliongozwa na roho ya Mungu kutabiri hivi: “Zitakoma.” (1 Wakorintho 13:8) Hivyo basi, tunaweza kujua jinsi gani kwamba mtu ana roho takatifu leo?

Ni Nani kwa Kweli Wana Roho Takatifu Leo?

Yesu alijua kwamba zawadi ya kusema kwa lugha mbalimbali ingekoma muda mfupi baada ya kufanyizwa kwa kutaniko la Kikristo. Punde kabla ya kifo chake, Yesu alitaja ishara yenye kudumu ambayo ingewatambulisha wafuasi wake wa kweli. Alisema: “Kwa jambo hili wote watajua kwamba ninyi ni wanafunzi wangu, mkiwa na upendo kati yenu wenyewe.” (Yohana 13:35) Katika ule mstari ambapo Neno la Mungu linatabiri kuwa zawadi za kimuujiza zingekoma hatimaye, tunasoma: “Upendo haushindwi kamwe.” —1 Wakorintho 13:8.

Upendo umeorodheshwa wa kwanza kati ya sehemu tisa za “matunda” ya roho takatifu ya Mungu. (Wagalatia 5:22, 23) Kwa hiyo, wale ambao kwa kweli wana roho ya Mungu—na hivyo wanaungwa mkono na Mungu—wangependana kikweli. Zaidi ya hayo, sehemu ya tatu ya matunda ya roho ni amani. Kwa hiyo, wale walio na roho takatifu leo wangekuwa watu wenye kujitolea kudumisha amani, wanaojitahidi sana kuepuka mambo kama imani kali, ubaguzi, na ujeuri.

Pia, kumbuka unabii wa Yesu katika Matendo 1:8. Alitabiri kwamba wanafunzi wake wangepokea nguvu ili wawe mashahidi wake “mpaka sehemu ya mbali zaidi na dunia.” Yesu pia alisema



kwamba kazi hiyo ingeendelea “hata mwisho wa dunia.” (Mathayo 28:20, *Zaire Swahili Bible*) Hivyo, kazi hii ya kuhubiri duniani kote ingeendelea kuwa ishara ya kuwatambulisha wale ambao kwa kweli wana nguvu ya roho takatifu.

Una maoni gani? Ni kikundi gani cha watu ambacho unaona kwa kweli kina roho takatifu leo? Ni nani wanaoonyesha matunda ya roho, hasa upendo na amani, kiasi kwamba wanateswa na serikali kwa sababu wanakataa kupigana vita katika jeshi lolote duniani? (Isaya 2:4) Ni nani wanaojitahidi kuepuka kazi za mwili, kama vile uasherati, na hata kuwaondoa kati yao watu wenye mazoea hayo ambao hawatubu? (1 Wakorintho 5:11-13) Ni nani wanaohubiri ulimwengu kote habari njema kwamba Ufalme wa Mungu ndilo tumaini pekee kwa wanadamu? —Mathayo 24:14.

Wachapishaji wa gazeti hili hawana shaka kusema kwamba Mashahidi wa Yehova ndio watu ambao, kupatana na maelezo ya Biblia, wana roho takatifu. Tunakutia moyo uwajue vizuri zaidi na ujiamulie mwenyewe kama kwa kweli wanaungwa mkono na Mungu.



Kwa nini wanadamu tu ndio husali? ONA UKURASA WA 3.



Je, kwa kweli Mungu anasikiliza na kujibu sala zetu?

ONA UKURASA WA 11.



Kuna tofauti gani kati ya jinsi Yesu alivyowaponya watu na jinsi wale wanaodai kuwaponya watu kimuujiza leo wanavyofanya? ONA UKURASA WA 13.



Biblia inaweza kutusaidia jinsi gani kushinda hisia zisizofaa?

ONA UKURASA WA 19.



Je, roho takatifu ni mtu? ONA UKURASA WA 26.

Je, ungependa kutembelewa?